NOVEMBA 3, 2026


/islamicftz

VISION 2050

IMAAN

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

ISSN 5618 - NO. 609



Msikiti wa Al Ghaith Moro kuanza kuswaliwa Ijumaa Novemba 6

Msukumo mpya Z'bar kuwa kitovu huduma fedha za Kiislamu

CIFCA, ZIAAT, SUZA zabeba ajenda Fedha za Halal



Makubaliano yakisainiwa na Makamu Mwenyekiti wa CIFCA, Prof. Mohammed Hafidh, na Mkurugenzi Mtendaji wa ZIAAT, CPA Ame B. Shadhil, huku Katibu Mkuu wa CIFCA, Salum Shaban Lupande, akishuhudia.

Lupande: Elimu ya fedha ipimwe kwa mabadiliko kwa wananchi

MAADHIMISHO

Miaka 70 ya Usajili Jumuiya za Kiraia



Ziara za Dkt Mwinyi zinavyozalisha fursa mpya kwa Zanzibar



Shule zote 3 za Imaan zapata ufaulu daraja 'A'

- Banda la The Islamic Foundation lilivyofurika
- Viongozi wa Kikristo wagawiwa Qur'an, watoa neno
- Aref Nahdi asifu Serikali kulinda uhuru wa kuabudu
- Rais Samia ataka jumuiya za dini kulinda maadili ya Taifa

Mshikamano ugeuke kuwa hatua za kulinda maisha, haki za Wapalestina

Msikiti wa Al Ghaith Morogoro kuanza kuswaliwa Ijumaa Novemba 6

NA
Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

Msikiti wa Al Ghaith, unaomilikiwa na taasisi ya The Islamic Foundation, unatarajiwa kuanza kuswaliwa Swala ya Ijumaa, Novemba 6, 2026, kabla ya kufunguliwa rasmi Januari mwakani. Akitoa taarifa hiyo, Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Sheikh Aref Nahdi, alisema kila kitu kipo tayari kwa ajili ya kutumika.

Msikiti huo utakuwa mkubwa na mzuri zaidi mkoani Morogoro.

Alisema ufunguzi rasmi unatarajiwa kufanyika Januari 2027, kabla ya kuanza kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani 1448 Hijria, huku wageni wengi wakitarajiwa kuhudhuria.

Kwa mujibu wa Nahdi, Al Ghaith hautakuwa msikiti kwa ajili ya ibada pekee, bali pia utakuwa ni kituo kitakachotoa huduma cha huduma mbalimbali za kidini, ikiwemo mihadhara.

Alisema uzuri na ukubwa wa msikiti huo utaufanya uwe kivutio cha kipekee mkoani Morogoro.



JUMADA AL-AWWAL 23, 1448

HABARI NA
DAR ES SALAAM
Na mwandishi wetu



Shule zote 3 za Imaan zapata ufaulu daraja ‘A’

PSLE 2026 EXAMINATION RESULTS

IMAAN PRIMARY SCHOOL - PS1104047

WALIOFANYA MTIHANI : 74
WASTANI WA SHULE : 273.0000 DARAJA A (BORA)

MADARAJA YA UFAULU WA UJUMLA

JINSI	A	B	C	D	E
WASICHANA	34	0	0	0	0
WAVULANA	40	0	0	0	0
JUMLA	74	0	0	0	0

Shule za Msingi za Imaan Morogoro, Dodoma Imaan, na Mafia Imaan zinayomilikiwa na Taasisi ya The Islamic Foundation, zimeweka rekodi ya kipekee ya kitaaluma baada ya wanafunzi wake wote waliohitimu Darasa la Saba mwaka 2026 kupata Daraja la Kwanza (A), na hivyo kufikisha asilimia 100 ya ufaulu.

Kwa mujibu wa matokeo hayo yaliyotangazwa Novemba 3, 2026 na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Profesa Saidi Mohamed, yanaifanya shule hizo kuendelea kuthibitisha uwezo wake katika kutoa elimu bora na kuzalisha wahitimu wenye kiwango cha juu cha ufaulu.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Profesa Said Mohamed, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu matokeo ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi

Mafanikio hayo ni kielelezo cha juhudi za muda mrefu katika uwekezaji wa elimu, usimamizi thabiti wa ufundishaji na ujifunzaji, pamoja na kuweka mazingira yanayowawezesha wanafunzi kutambua na kukuza uwezo wao kitaaluma.

Ufaulu wa wanafunzi wote kupata Daraja la Kwanza unaweka alama muhimu katika historia ya shule hizo, huku ukidhihirisha umuhimu wa ushirikiano baina ya walimu, wazazi na wanafunzi katika kufanikisha malengo ya elimu.

Mbali na mafanikio ya kitaaluma, Shule za Msingi Imaan zimeendelea kusimamia falsafa ya elimu inayounganisha maarifa na malezi, kwa kuzingatia misingi ya maadili ya Kiislamu, nidhamu na uwajibikaji.

Mfumo huo unalenga kumjenga mwanafunzi asiye na uwezo wa kufaulu mitihani pekee, bali pia mwenye misingi imara ya kimaadili, nidhamu na utayari wa kukabiliana na changamoto za maisha.

Kwa mtazamo huo, matokeo ya mwaka huu yanaongeza uzito wa nafasi ya shule hizo katika sekta ya elimu, yakionyesha kuwa ubora wa elimu hauishii katika matokeo ya mitihani, bali pia unahusisha malezi na maandalizi ya kizazi chenye maarifa na maadili.

Mafanikio hayo pia yanatoa ujumbe kwa wadau wa elimu kuhusu umuhimu wa kuwekeza katika walimu wenye weledi, mazingira bora ya kujifunzia na mifumo madhubuti ya usimamizi wa taaluma.

Kwa Shule za Msingi Imaan, kufaulisha wanafunzi wote kwa Daraja la Kwanza si mafanikio ya kundi la wahitimu pekee, bali ni ushahidi wa juhudi za pamoja zinazolenga kuifanya elimu kuwa nyenzo ya kujenga jamii yenye maarifa, nidhamu na maadili mema.

NA
Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

Msukumo mpya Z’bar kuwa kitovu huduma fedha za Kiislamu



☞ Mafanikio ya elimu ya fedha yapimwe kwa mabadiliko ya wananchi — Lupande

CIFCA, ZIAAT kuimarisha taaluma huduma fedha za Kiislamu Zanzibar

Juhudi za kuimarisha sekta ya fedha za Kiislamu Zanzibar zimepata msukumo mpya baada ya Kituo cha Uzingatiaji wa Sharia na Ushauri wa Fedha za Kiislamu (CIFCA) na Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri wa Kodi Zanzibar (ZIAAT) kusaini makubaliano ya miaka minne ya kujenga uwezo wa wataalamu.

Makubaliano hayo yalisainiwa Oktoba 28, 2026, na Makamu Mwenyekiti wa CIFCA, Prof. Mohammed Hafidh, na Mkurugenzi Mtendaji wa ZIAAT, CPA Ame B. Shadhil, huku Katibu Mkuu wa CIFCA, Salum Shaban Lupande, akishuhudia.

Ushirikiano huo unalenga kuimarisha utaalamu katika huduma za fedha zinazozingatia Sharia, uhasibu, ukaguzi, kodi, usimamizi wa vihatarishi na uandaaji wa taarifa za fedha.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Hafidh alisema maendeleo ya sekta yanahitaji wahasibu wanaoelewa miamala, wakaguzi wanaoweza kutathmini ushahidi na wasimamizi wenye uwezo wa kubaini mapungufu na kuhakikisha yanarekebishwa.

Alisema utaalamu huo ni muhimu kujenga imani ya wananchi na wawekezaji kwamba huduma zinazotangazwa kuwa za Kiislamu zinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya Sharia.

Prof. Hafidh alieleza kuwa makubaliano hayo yanarasimisha ushirikiano uliokwishaanza kati ya taasisi hizo. “Safari ilishaanza,” alisema, akisisitiza umuhimu wa kuhakikisha ushirikiano huo unazalisha matokeo yanayoonekana.

Aliipongeza ZIAAT kwa juhudi za kuwajengea uwezo wanachama wake, huku akiwasilisha salamu za Mwenyekiti wa CIFCA, Sheikh Aref Nahdi.

Kwa upande wake, CPA Ame Shadhil alisema ushirikiano huo utawezesha mafunzo, kubadilishana maarifa na kushirikiana katika tafiti.

Zanzibar kuelekea viwango vya kimataifa

Sehemu muhimu ya makubaliano ni maandalizi ya matumizi ya viwango vya kimataifa vya fedha za Kiislamu vinavyoandaliwa na Shirika la Uhasibu na Ukaguzi wa Taasisi za Fedha za Kiislamu (AAOIFI), lenye makao makuu Bahrain.

Katibu Mkuu wa CIFCA, Salum Lupande, alisema ZIAAT tayari imewasilisha maombi rasmi ya uanachama wa AAOIFI, huku CIFCA ikiendelea kusaidia mawasiliano na maandalizi ya mafunzo kuhusu viwango hivyo.

Juhudi hizo zilianza mwaka 2024 na kuendelezwa kupitia mazungumzo yaliyofanyika Bahrain, Aprili 2025. CIFCA ilisaidia ZIAAT kuandaa maombi ya kujenga uwezo na kushirikisha mamlaka za Serikali.

Prof. Hafidh alisisitiza kuwa matumizi rasmi ya viwango hivyo yatahitaji ushirikishwaji wa mamlaka husika na kufuata taratibu za kisheria.

Mafunzo Tanzania Bara na Zanzibar

Makubaliano yanahusisha programu mbili za pamoja kila mwaka, moja Zanzibar na nyingine Tanzania Bara, zikiwemo semina, warsha, kozi fupi na mafunzo endelevu ya kitaaluma.

CIFCA itatumia uzoefu wake na mitandao ya kimataifa kusaidia upatikanaji wa wakufunzi, nyenzo na maarifa mapya. Pia ina uzoefu wa kuratibu mafunzo na mitihani ya AAOIFI nchini Tanzania.

Timu ya pamoja itaundwa kuratibu utekelezaji, kubaini mahitaji ya mafunzo na kutoa taarifa za maendeleo kila baada ya miezi mitatu.

Prof. Hafidh alisisitiza umuhimu wa kupima mafanikio kwa shughuli zilizotekelezwa, watu walionufaika na matumizi halisi ya maarifa yaliyopatikana.

Aidha, alihimiza waajiri na taasisi za fedha kusaidia wataalamu kushiriki mafunzo, huku akisisitiza uwazi wa bajeti na uwajibikaji.

Ushirikiano huo unatarajiwa kujenga wataalamu wenye uwezo wa kutumia viwango vya kimataifa na kuendeleza maarifa ndani ya taasisi zao, hatua inayoweza kuimarisha nafasi ya Zanzibar katika safari ya kuwa kitovu cha huduma za fedha za Kiislamu Afrika Mashariki.



Lupande: Elimu ya fedha ipimwe kwa mabadiliko kwa wananchi

Mafanikio ya programu za elimu ya fedha nchini yanapaswa kupimwa kwa mabadiliko ya maarifa, mitazamo na tabia za wananchi katika kusimamia fedha zao, badala ya kuangalia idadi ya watu waliohudhuria mafunzo pekee.

Hayo yamesemwa na Salum Shaban Lupande, mwakilishi wa Chama cha Waelimishaji wa Fedha Waliothibitishwa Tanzania (ACFET), katika warsha ya kujadili Mwongozo wa Utekelezaji wa Programu za Elimu ya Fedha, iliyoandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Oktoba 29, 2026.

Warsha hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Kilimanjaro, ofisi za BoT, Dar es Salaam, kwa kushirikisha waelimishaji wa fedha na wadau wa sekta hiyo.

Lupande, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum iliyoundwa na BoT ya kupitia Mtaala wa Watoa Elimu ya Fedha nchini, alisema elimu ya fedha inapaswa kuwasaidia wananchi kupanga matumizi, kuweka akiba, kukopa kwa uwajibikaji, kutambua hatari za kifedha na kufanya maamuzi sahihi.


Alieleza kuwa upatikanaji wa huduma za kifedha pekee hautoshi ikiwa wananchi hawana maarifa ya kuzitumia ipasavyo.

Akizungumzia mwongozo huo ulioandaliwa na BoT kwa kushirikiana na wadhibiti wengine, Lupande alisisitiza umuhimu wa weledi, uaminifu, uwazi na kuepuka migongano ya maslahi katika utoaji wa elimu ya fedha.

Alipendekeza kuimarishwa kwa ushirikiano kati ya ACFET, Benki Kuu na wadau wengine, pamoja na kuweka mfumo endelevu wa mawasiliano na ushauri wa kitaalamu kwa waelimishaji.

Lupande, ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Kituo cha Uzingatiaji wa Sharia na Ushauri wa Huduma za Fedha za Kiislamu (CIFCA), alisisitiza umuhimu wa mifumo rahisi ya utoaji taarifa na ufuatiliaji wa programu hizo.

Alisema lengo kuu ni kuhakikisha elimu inayotolewa inachangia kuboresha ustawi wa kifedha wa Watanzania.





Sheikh Mohammad Issa: Msifanye watoto mtaji wa uzeeni, wekeni akiba

Watanzania wametahadharishwa dhidi ya tabia ya kutumia mapato yao bila mipango na kutegemea watoto kuwahudumia watakapokuwa wazee, badala ya kuweka akiba na kuwekeza wakati bado wana uwezo wa kufanya kazi.

Tahadhari hiyo imetolewa na mtaalamu wa fedha za Kiislamu, Sheikh Muhammad Issa, katika semina ya mtandaoni iliyoandaliwa na kampuni ya Yusra Sukuk Company Limited, Jumamosi, Oktoba 31, 2026, yenye mada "Ujue Uwekezaji Halali katika Hisa."

Sheikh Issa alisema watu wengi wanajishughulisha na mahitaji ya kila siku bila kutenga fedha kwa ajili ya maisha yao ya baadaye, hali inayoweza kuwaweka katika mazingira magumu wanapozeeka na uwezo wao wa kufanya kazi kupungua.

"Sisi Watanzania hatuna tabia ya kutunza fedha. Lile somo zima katika Surah Yusuf lile, lile somo la la akiba, hatuna sisi! Sisi ni from hand to mouth (mkononi hasi mdomoni)," Sheikh Issa alisema.

Akisisitiza umuhimu wa kujitegemea kifedha uzeeni, alisema watoto ni mtaji mbaya wa kutegemewa.

"Usiweke mtaji kwamba ni watoto umewasomesha. Watoto hizo ni entities nyingine, ni kampuni na zenyewe, zenye sheria zake. Hao watakuwa hata kama umewasomesha, watao; wakishaooa wanaangalia wake zao na watoto wao, ada za shule, sijui kodi ya nyumba, sijui vitu gani. Wewe ndio umezeeka unawategemea, utawalaani tu!" alisema.

"Jiwekee akiba kwenda kwenye uzee wako kwa njia kama hizi za uwekezaji kwenye hisa, kwenye Sukuk, kwenye mifuko ya halali na vitu vya namna hiyo," alisema.

Matumizi ya machungwa na karanga

Akizungumzia matumizi yasiyo na mipango, Sheikh Issa alisema baadhi ya Watanzania wamejenga mazoea ya kutumia fedha kwa vitu vidogo bila kuzingatia bajeti, jambo linalopunguza uwezo wao wa kuweka akiba.

Alitoa mfano wa mtu anayeondoka nyumbani kwenda mjini na njiani kununua machungwa, kisha anapokutana na muuzaji wa karanga ananunua tena, bila kuwa na mpango wa matumizi hayo.

"Yale machungwa, karanga, sijui vitu gani ulivyokuwa unanunua kutwa nzima, ulivi-wekea bajeti? Vinatoka kwenye mfuko gani vile?" alihoji.

Aliongeza: "Ukivikusanya hivyo vyote vidogo vidogo ukaviongeza na wale wanaovuta sigara kwa mfano, unaona, mwingine anavuta sigara, mwingine anakula na mirungi, anavuta sigara anakula na mirungi, na bado analalamika yeye maskini. Umaskini mwingine tunautaka wenyewe!"

Alisema fedha zinazotumika kwa namna hiyo, zikikusanywa na kuwekezwa kidogo kidogo, zinaweza kumsaidia mtu kujenga mtaji wa muda mrefu.

Hisa na Sukuk kama njia za uwekezaji

Akieleza namna wananchi wanavyoweza kujenga akiba, Sheikh Issa alisema uwekezaji katika hisa unaweza kuanza kwa kiasi kidogo cha fedha, tofauti na baadhi ya bidhaa za Sukuk zinazohitaji kiwango kikubwa zaidi cha kuanzia.

Alitoa mfano wa mtu anayeweza kununua hisa zenye thamani ya Sh40,000, Sh50,000 au Sh100,000, kutegemea bei ya hisa na gharama za ununuzi.

Waislamu waonywa si kila hisa ni halali kwa Muislamu kuwekeza

Waislamu wametakiwa kuchunguza shughuli za kampuni kabla ya kununua hisa zake, kwani si kila uwekezaji katika soko la mitaji unakidhi misingi ya Sharia.

Wito huo umetolewa na Sheikh Muhammad Issa katika darasa la mtandaoni kuhusu uwekezaji halali katika hisa, lililoandaliwa na kampuni ya Yusra Sukuk, Jumamosi, Oktoba 31, 2026.

Sheikh Issa alisema uhalali wa hisa unategemea aina ya biashara inayofanywa na kampuni pamoja na uzingatiaji wake wa kanuni za fedha za Kiislamu.

Akizungumzia sekta ya benki, aliitaja Amana Bank kuwa mfano wa benki inayofuata misingi ya Sharia, huku akieleza kuwa benki nyingine zenye madirisha ya huduma za Kiislamu zinahitaji uchunguzi wa ziada kabla ya hisa zake kuzingatiwa kwa uwekezaji.

Alisema uchunguzi huo, unaojulikana kama Sharia screening, unasaidia kubaini kama kampuni inakidhi vigezo vya uwekezaji halali.

Aidha, Sheikh Issa alieleza kuwa hisa humpa mwekezaji umiliki katika kampuni, fursa ya kupata gawio na kunufaika na ongezeko la thamani.

Hata hivyo, alitahadharisha kuwa gawio halijahakikishwa na bei za hisa zinaweza kupanda au kushuka kulingana na mwenendo wa soko. Aliwahimiza wawekezaji kuel ewa shughuli za kampuni, hali yake ya kifedha na sera ya gawio kabla ya kuwekeza.

JUMADA AL-AWWAL 23, 1448

HABARI DODOMA NA

Na mwandishi wetu



Samia atimiza ndoto

Ndoto ya miaka 53 ya kuifanya Dodoma makao makuu ya Serikali yatimia, yaingia kwenye rekodi za nchi ya tatu Afrika.

Kuzinduliwa kwa majengo ya wizara na taasisi za Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma kunatarajiwa kuwezesha wananchi kunufaika na urahisi wa huduma, kupungua kwa gharama za kufuatilia shughuli za kiutawala na kuongezeka kwa fursa za biashara.

Kujengwa kwa ofisi hizo katika eneo moja kunaelezwa kutarahisisha uratibu wa shughuli za Serikali na mawasiliano kati ya wizara na taasisi, pamoja na kupunguza muda unaotumika kufikisha nyaraka na kushughulikia masuala ya wananchi.

Kwa wananchi wanaohitaji huduma kutoka taasisi mbalimbali za Serikali, hatua hiyo inatarajiwa kupunguza usumbufu na gharama za kusafiri kutoka eneo moja kwenda jingine. Wakati huohuo, wafanyabiashara na watoa huduma wanatarajiwa kupata fursa mpya kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiutawala na watu wanaofika katika eneo hilo.

Akizungumza wakati wa kuzindua majengo na miundombinu ya Mji wa Serikali Mtumba, Rais Samia Suluhu Hassan alisema Serikali imewekeza katika mazingira ya kisasa ya kufanyia kazi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi kwa watumishi wa umma.

Alisema majengo hayo yamejengwa kwa fedha za ndani bila kutegemea mikopo kutoka taasisi yoyote, hivyo amewataka watumishi wa umma kutumia mazingira hayo bora kuwahudumia wananchi kwa heshima, uadilifu na ufanisi.

“Tumepata majengo na miundombinu mizuri, imara na ya kisasa tuliyojenga kwa fedha zetu wenyewe. Sasa tukawahudumie wananchi kwa ufanisi mkubwa, tunaamini huduma zitatolewa kwa viwango zaidi na kasi,” alisema Rais Samia.

Hata hivyo, Rais Samia alisisitiza kuwa kuhamishia shughuli za Serikali Dodoma hakupaswi kuwa sababu ya wananchi kutoka mikoa mbalimbali kusafiri hadi makao makuu kufuata huduma zinazoweza kupatikana katika maeneo wanayoishi.

Alisema mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) inapaswa kuunganishwa ili taarifa za mwananchi zinazopokelewa na taasisi moja ziweze kutumiwa na nyingine bila kumtaka kuziwasilisha mara kwa mara.

> **“Mradi huu tumejenga kwa fedha zetu za ndani, bila kutegemea mikopo kutoka taasisi za fedha. Hivyo, watumishi wa umma watumie mazingira bora ya kazi yaliyowekwa ili kuongeza uwajibikaji, uadilifu na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.”**
> ***Rais Samia***

“Mathalan, mwananchi kutoka Rukwa, Kagera, Mtwara au Kigoma asitumie muda na fedha nyingi kuja kufuatilia jambo lake ambalo lingeweza kushughulikiwa huko huko aliko,” alisema.

Aliongeza kuwa mifumo ya Serikali inapaswa kuunganishwa ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao na kupunguza ulazima wa wananchi kufika Dodoma kwa kila jambo.



MAGUFULI

Alifufua kwa nguvu utekelezaji wa mpango wa kuhamisha shughuli za Serikali mwaka 2016. Magufuli alitangaza kuhamia rasmi Dodoma kutoka Dar Oktoba 12, 2019.



RAIS SAMIA

Rais Samia amezindua majengo ya ofisi za wizara na taasisi za Serikali pamoja na barabara za lami katika Mji wa Serikali Mtumba. Kwa uzinduzi huo Rais Samia amekamilisha ndoto ya Mwalimu Nyerere na kazi iliyoanzishwa na mtangulizi wake, JPM



Ziara za Mwinyi zinavyozalisha fursa mpya visiwani Zanzibar

Ziara ya kikazi ya siku nne nchini Korea Kusini ya Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi, imefungua fursa za ushirikiano katika sekta ya nishati, uwekezaji na utalii, huku Zanzibar ikipata nafasi ya kuwa mwenyeji wa Jukwaa la Kimataifa la Sera za Utalii kwa Visiwa (ITOP) mwaka 2027.

Miongoni mwa matokeo ya ziara hiyo ni mazungumzo kuhusu suluhisho la kudumu la changamoto ya umeme Zanzibar, kuvutia kampuni za Korea Kusini kuwekeza katika miradi ya kimkakati na kukabidhiwa bendera ya uenyeji wa ITOP 2027.

Ziara hiyo ilianza Oktoba 27, 2026, Rais Mwinyi akiwa ameambatana na mkewe, Mama Mariam Mwinyi, na ujumbe wake. Ilikamilika Oktoba 30, 2026, jijini Seoul.

Mchambuzi wa Diplomasia na Uchumi wa Kimataifa, Haji Salum, amesema Korea Kusini ni nchi ambayo Zanzibar inaweza kujifunza uzoefu wake wa maendeleo ya viwanda na uchumi wa bahari.

"Korea Kusini imetoka kwenye umaskini hadi kuwa taifa la teknolojia kwa miaka 40 tu kwa kutumia bahari na viwanda. Zanzibar inajaribu kuiga mfumo huo. Mazungumzo ya umeme na WG Corporation na Posco yanaonesha Zanzibar inataka kujitoa kwenye utegemezi wa umeme wa Bara," amesema.

Kwa upande wake, mchambuzi wa utalii na uchumi wa buluu, Asmaa Saidi, amesema kukabidhiwa uenyeji wa ITOP 2027 ni fursa ya kuitangaza Zanzibar kimataifa.

Hata hivyo, amesema ni muhimu kuhakikisha miradi ya Mice na Hospitali ya Binguni inayozungumziwa na kampuni za Heerim na Samoo inatekelezwa kwa wakati.

Naye mchambuzi wa nishati na miundombinu, Haroub Mohamed, amesema mipango ya kuimarisha upatikanaji wa umeme na kurejesha reli inaweza kusaidia kuvutia viwanda na kukuza utalii. "Zanzibar haiwezi kuvutia viwanda na utalii wa hali ya juu kama umeme ni wa kukatika na usafiri ni wa magari tu. Kama Korea itawekeza kwenye gridi ndogo za umeme wa jua na upepo pamoja na reli ya utalii, gharama za uzalishaji zitashuka na ajira za vijana zitaongezeka," amesema.

Kwa upande wa wananchi, mvuvi na mkulima wa mwani kutoka Paje, Ali Juma, amesema ana matumaini ushirikiano huo utasaidia kuongeza thamani ya mwani na kipato cha wakulima.

"Kama Rais ameenda Korea na kuona jinsi mwani unavyochakatwa kuwa chakula na vipodozi, basi alete huo mtambo hapa Zanzibar, tunataka bei ipande," amesema.

Mfanyabiashara wa utalii kutoka Forodhani, Mwanaisha Khamis, amesema uenyeji wa ITOP 2027 ni fursa kwa wafanyabiashara wadogo, lakini amesisitiza umuhimu wa kuboresha huduma za maji na umeme kabla ya wageni kuwasili.

"Hii mikataba ya Korea ya maji na umeme itekelezwe haraka, sio makaratasi tu," amesema.

سَبْعُونَ

NA
Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

MIAKA 70 YA USAJILI WA JUMUIYA ZA KIRAIA

Rais Samia aitunuku The Islamic Foundation kwa huduma kwa jamii



Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameipatia Taasisi ya The Islamic Foundation tuzo ya kutambua mchango wake katika kuboresha maisha ya wananchi kupitia huduma za kijamii na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo nchini.

Tuzo hiyo imekabidhiwa kwa Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Aref Nahdi, na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Patrobas Katambi, wakati wa maadhimisho ya miaka 70 ya Usajili wa Jumuiya za Kiraia yaliyofanyika katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Utambuzi huo unaakisi mchango wa taasisi hiyo katika sekta mbalimbali zikiwamo elimu, afya, maji, huduma za kidini na ustawi wa makundi yenye uhitaji, kupitia miradi inayolenga kupunguza changamoto za kijamii na kuongeza fursa za maendeleo.

Katika sekta ya maji, The Islamic Foundation imekuwa ikitekeleza miradi ya uchimbaji wa visima vya maji safi na salama katika maeneo yenye uhaba wa huduma hiyo, hatua inayosaidia kupunguza umbali na muda unaotumiwa na wananchi kutafuta maji.

Katika elimu, taasisi hiyo imewekeza katika ujenzi na uendeshaji wa shule za msingi na sekondari, kwa lengo la kuongeza fursa za kupata elimu bora kwa watoto na vijana.

Pamoja na hayo, imekuwa ikiendesha programu za kusaidia yatima na makundi yenye uhitaji maalumu, kutoa misaada kwa waathirika wa majanga mbalimbali na kushiriki katika shughuli za kibinadamu zinazolenga kuwafikia wananchi wanaokabiliwa na changamoto za maisha.

Katika eneo la huduma za kidini, taasisi hiyo imechangia ujenzi wa misikiti na kuboresha mazingira ya ibada, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuimarisha huduma za kiroho na kijamii.

Maadhimisho hayo ya miaka 70 yalilenga kutambua na kuthamini mchango wa jumuiya za kiraia katika kusaidia Serikali kuboresha huduma kwa wananchi na kuharakisha maendeleo ya taifa.

Tuzo hiyo inaongeza utambuzi wa mchango wa The Islamic Foundation katika kutumia taasisi za kijamii kama nyenzo ya kuleta mabadiliko chanya na kugusa maisha ya wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

سَبْعُونَ

NA
Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

MIAKA 70 YA USAJILI WA JUMUIYA ZA KIRAIA



Banda la The Islamic Foundation lafurika maonesho ya jumuiya za kiraia

Zaidi ya wageni 1,900 wametembelea banda la The Islamic Foundation (TIF) katika maadhimisho ya miaka 70 ya Usajili wa Jumuiya za Kiraia nchini, huku ugawaji wa tafsiri za Qur'an na vitabu vingine vya dini bila malipo ukiwa miongoni mwa vivutio vikuu.

Maadhimisho hayo, yaliyofanyika Oktoba 28–30, 2026, katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam, yalishirikisha taasisi na jumuiya mbalimbali kutoka maeneo tofauti nchini.

Katika maonesho hayo, The Islamic Foundation iligawa tafsiri za Qur'an kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza pamoja na Juzuu Amma, ikiwa ni sehemu ya juhudi zake za kueneza elimu ya Uislamu na kuongeza uelewa wa jamii kuhusu mafundisho ya dini hiyo.

Banda la taasisi hiyo lilitembelewa na viongozi wa dini mbalimbali, wawakilishi wa jumuiya za kiraia na wananchi waliohudhuria maadhimisho hayo.

Baadhi ya wageni walipokea nakala zaidi za vitabu kwa ajili ya kuwafikishia watu wengine katika maeneo wanayotoka, hatua iliyopanua wigo wa usambazaji wa machapisho hayo nje ya ukumbi wa maonesho.

Mbali na ugawaji wa vitabu, banda hilo lilitoa fursa kwa wageni kufahamu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na The Islamic Foundation katika sekta za elimu, afya, maji, malezi na huduma za kijamii.

Ushiriki huo uliipa taasisi nafasi ya kutambulisha mchango wake katika maendeleo ya jamii, huku ikikutana na viongozi na wadau kutoka taasisi nyingine kwa ajili ya kubadilishana uzoefu.

Miongoni mwa waliovutiwa na huduma ya ugawaji wa vitabu walikuwa viongozi wa dini ya Kikristo, ambao walipongeza utaratibu huo na kueleza kuwa unatoa fursa ya kujifunza mafundisho ya Uislamu kupitia maandiko yake.

Maadhimisho hayo yalifunguliwa Oktoba 28 na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Patrobas Katambi, yakihusisha takribani jumuiya na taasisi 2,000.

Mkutano ulifungwa Ijumaa saa tano asubuhi ili kuwawezesha washiriki Waislamu kujiandaa kwa Swala ya Ijumaa.

سَبْعُونَ

NA
Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

MIAKA 70 YA USAJILI WA JUMUIYA ZA KIRAIA

Viongozi wa Kikristo: Qur'an isomwe kuondoa dhana potofu kuhusu Uislamu

Viongozi wa dini ya Kikristo nchini wamepongeza juhudi za The Islamic Foundation za kugawa tafsiri za Qur'an bila malipo, wakisema hatua hiyo inatoa fursa kwa watu wa imani tofauti kuufahamu Uislamu kupitia maandiko yake badala ya kutegemea propaganda na dhana potofu.

Wakizungumza na Gazeti Imaan katika maadhimisho ya miaka 70 ya Usajili wa Jumuiya za Kiraia yaliyofanyika Mlimani City, Dar es Salaam, viongozi hao wamesema kusoma vitabu vya dini nyingine kunasaidia kujenga uelewano, upendo na kuheshimiana.

Askofu Andrew Wagana amesema alishangazwa kugawiwa vitabu hivyo bila malipo, kwani awali alidhani vinauzwa.

"Haya ni maajabu, kugawiwa vitabu vya kidini bure. Sisi tulijua vitabu hivi vinauzwa, lakini tumefurahi kuona vinatolewa bila malipo. Hii ni fursa nzuri ya kujifunza na kuifahamu dini ya Kiislamu," amesema.

Mchungaji Elias Lunyarila naye amesema hakutarajia kupata tafsiri za Qur'an bila malipo,



akieleza kuwa ukarimu huo utawapa watu wengi nafasi ya kusoma na kuelewa mafundisho ya Uislamu.

Kwa upande wake, Askofu Andrew Baraka amesema hatua hiyo inapaswa kuigwa na taasisi nyingine, kwa kuwa inawasaidia wananchi kujifunza kuhusu Uislamu na kuondoa mitazamo isiyo sahihi.

Kauli hiyo imeungwa mkono na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Kanisa la AGCCI, Elia William Mashaka, aliyesema ni muhimu kwa waliopokea vitabu hivyo kuvisoma ili kupata uelewa sahihi wa dini ya Kiislamu.

Mashaka amesema ugawaji wa vitabu hivyo unaonyesha namna ukarimu na upendo vinavyoweza kuimarisha mahusiano baina ya waumini wa dini tofauti.

Naye Askofu Asher Agostino Bango amesema tafsiri za Qur'an kwa Kiswahili na Kiingereza, pamoja na Juzuu Amma, zitawawezesha watu wengi kuelewa ujumbe wa Qur'an na kuwashirikisha wengine maarifa watakayopata.

"Tukifahamu yaliyomo ndani ya vitabu hivi, itatusaidia kuwa mabalozi kwa wenzetu na kuwaeleza kile tulichokisoma, hivyo kuondoa dhana potofu na kuujua Uislamu wa ukweli kupitia mafundisho yake," amesema.

Mchungaji Elia Mtuna amesema ugawaji wa vitabu hivyo umempa fursa ya kujifunza zaidi kuhusu Uislamu, huku akipongeza ukarimu wa The Islamic Foundation.

Kwa upande wake, Mchungaji Dkt. Daniel John amesisitiza umuhimu wa kujifunza mafundisho ya dini nyingine, akisema kufanya hivyo kunasaidia kujenga uelewano na kuheshimiana katika jamii.



سَبْعُونَ

NA
Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

MIAKA 70 YA USAJILI WA JUMUIYA ZA KIRAIA



Aref Nahdi asifu Serikali kwa kulinda uhuru wa kuabudu

Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi, ameipongeza Serikali kwa kulinda uhuru wa kuabudu na kuweka mazingira yanayowezesha jumuiya za kiraia kutekeleza shughuli zake, ikiwemo kutoa huduma za kijamii na kuchangia maendeleo ya taifa.

Aref ametoa pongezi hizo wakati wa maadhimisho ya miaka 70 ya Usajili wa Jumuiya za Kiraia nchini, yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Amesema uhuru wa kuabudu ni msingi muhimu wa amani, mshikamano na kuheshimiana katika jamii, hivyo kila mwananchi anapaswa kuwa na nafasi ya kufuata imani yake na kutekeleza ibada kwa mujibu wa misingi ya dini yake.

Ameeleza kuwa mazingira yanayotolewa na Serikali yamewezesha waumini wa dini mbalimbali kutekeleza shughuli zao za kiimani na kuimarisha mahusiano mema baina yao.

Aidha, ameipongeza Serikali kwa kuzipa jumuiya za kiraia nafasi ya kutekeleza majukumu yake, akisema taasisi hizo zina mchango mkubwa katika utoaji wa huduma za elimu, afya, maji, mazingira na kusaidia makundi yenye uhitaji.

Aref amesema ushirikiano kati ya Serikali na jumuiya hizo unaongeza wigo wa huduma kwa wananchi, hususan katika maeneo yenye mahitaji makubwa. Hata hivyo, amesisitiza kuwa uhuru huo unapaswa kwenda sambamba na uwajibikaji, uzingatiaji wa sheria na kuheshimu haki za wengine ili kudumisha amani na umoja wa kitaifa.

Maadhimisho hayo yamewakutanisha viongozi wa Serikali, viongozi wa dini na wadau mbalimbali kutambua mchango wa jumuiya za kiraia katika maendeleo na ustawi wa jamii.

MAKALA MAALUM



SHEIKH
Abadallah Saleh Ndauga
Mwenyekiti Hayatul Ulamaa



Mshikamano ugeuke kuwa hatua za kulinda maisha, haki za Wapalestina

Sehemu ya washiriki mkutano wa kujadili masuala ya Palestine uliondaliwa na Taasisi ya M A K. Masaajidi Ayadi Al kyer na kufanyika jijini Dar es Salaam kwa siku mbili, 29–30 Oktoba 2026

Nyuma ya kila habari kuhusu Palestina kuna mtoto anayetamani kesho yenye usalama, mama anayehofia maisha ya wanawe, familia inayotamani kurejea nyumbani, mwanafunzi anayesubiri kurudi shuleni na mgonjwa anayehitaji matibabu. Hawa ni watu wenye ndoto na matumaini, wanao-taka kuishi maisha ya kawaida yanayoheshimu haki na utu wao.

Mshikamano ugeuke kuwa hatua za kulinda maisha, haki za Wapalestina

Nyuma ya kila habari kuhusu Palestina kuna mtoto anayetamani kesho yenye usalama, mama anayehofia maisha ya wanawe, familia inayotamani kurejea nyumbani, mwanafunzi anayesubiri kurudi shuleni na mgonjwa anayehitaji matibabu.

Hawa ni watu wenye ndoto na matumaini, wanaotaka kuishi maisha ya kawaida yanayoheshimu haki na utu wao.

Kwa hiyo, suala la Palestina linavuka mipaka ya jiografia na siasa. Linagusa dhamiri ya binadamu na kutukumbusha wajibu wetu wa kutetea haki, heshima ya maisha, uadilifu na amani.

Mkutano wa kimataifa kuhusu Palestina nchini Tanzania unatoa nafasi ya kuimarisha wajibu huo. Tanzania, nchi yenye jamii zinazotofautiana kwa tamaduni na imani huku zikiishi pamoja, ni mahali panapofaa kutafakari umuhimu wa mshikamano kati ya watu na mataifa.

Juhudi za waandaaji wa mkutano, viongozi wa serikali, mabalozi, wanazuoni, viongozi wa dini, waelimishaji na washiriki wengine zinastahili kuthaminiwa. Ushiriki wao unaonesha umuhimu wa mazungumzo ya kimataifa na haja ya kuhakikisha kwamba suala la Palestina linaendelea kupewa uzito katika dhamiri ya dunia na ajenda za taasisi zake.

Hata hivyo, thamani ya mkutano huu itapimwa pia kwa hatua zitakazofuata. Tunayo nafasi ya kuhuisha dhamira yetu ya kibinadamu na kimaadili kwa watu ambao kwa muda mrefu wamekabiliwa na migogoro, kulazimika kuhama makazi yao na kukosa usalama. Watu hao wanaendelea kutamani maisha yenye uhuru, heshima na utulivu.

Jumuiya ya kimataifa ina wajibu wa kugeuza misingi inayotangaza kuwa vitendo. Maamuzi yanayofanywa yanapaswa kufuatiwa na hatua zinazotekelezeka, na mshikamano unaotamkwa unapaswa kuonekana katika juhudi zinazopunguza mateso na kulinda haki za binadamu.

Kutetea haki za Wapalestina ni jukumu la pamoja. Serikali, ujumbe wa kidiplomasia, taasisi za elimu, viongozi wa dini, asasi za kiraia na vyombo vya habari vina nafasi ya kuchangia. Mahusiano ya kimataifa pamoja na taasisi za kikanda na kimataifa yanapaswa kutumika kuimarisha haki na amani.

Katika kutimiza wajibu huo, maeneo matano yanahitaji kupewa kipaumbele.

Kwanza, ni muhimu kuunga mkono juhudi zote za dhati za kuwalinda raia, kukomesha mateso yao na kuhakikisha misaada ya kibinadamu inawafikia kwa usalama na kwa mwendelezo. Ulinzi wa maisha na utu wa watu unapaswa kuongoza maamuzi na hatua zinazochukuliwa.

Pili, ushirikiano wa kimataifa katika diplomasia na sheria unapaswa kuimarishwa ili kulinda haki halali za wananchi wa Palestina. Hii inajumuisha kuunga mkono haki yao ya kujiamulia mustakabali wao na kuanzisha taifa lao huru kwa mujibu wa sheria za kimataifa na maazimio husika ya Umoja wa Mataifa.

Tatu, kuna haja ya kuanzisha mipango ya pamoja ya elimu na utamaduni inayosaidia jamii kulielewa suala la Palestina. Taasisi za elimu na taaluma zinaweza kuchangia katika kukuza uelewa huo huku zikiimarisha misingi ya haki, amani na kuishi pamoja kwa kuheshimiana.

Nne, taasisi za dini na mashirika ya kibinadamu zinapaswa kuratibu juhudi zao katika utoaji wa misaada na shughuli za hisani. Ushirikiano huu uende sambamba na kuendeleza ujumbe unaoheshimu utu wa kila mtu na kukataa chuki na ubaguzi. Utetezi wa haki unapaswa kuimarisha ubinadamu wetu wa pamoja.

Tano, mkutano unapaswa kuweka utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yake. Maazimio yake yawe msingi wa programu, ushirikiano na shughuli endelevu zenye matokeo yanayoonekana. Huruma igeuke kuwa msaada, misimamo izae mipango, na matarajio yawe hatua zinazotekelezeka.

Amani ya kudumu inahitaji haki kuheshimiwa, watu kujisikia salama na kila mmoja kuwa na nafasi halisi ya kujenga maisha yake ya baadaye. Kukosekana kwa vita pekee hakutoshi kutimiza mahitaji hayo.

Ili amani idumu, mizizi ya mgogoro lazima ishughulikiwe na haki halali ziheshimiwe. Wananchi wa Palestina wanahitaji matumaini ya maisha yenye uhuru, heshima na utulivu.


Kwa msingi huo, utetezi wa Palestina unapaswa kuongozwa na dhamira ya kutafuta haki na amani inayolinda utu wa binadamu. Ujumbe wake uwe wa kujenga mshikamano na kupinga chuki na migawanyiko. Tunapozungumzia mateso ya Wapalestina, tunatetea pia msingi kwamba maisha ya kila binadamu yanastahili kulindwa na kuheshimiwa.

Kupita kwa muda hakupaswi kulifanya suala la Palestina lisahaulike. Mateso ya raia hayapaswi kuzoeleka, wala haki kupoteza thamani yake kwa sababu imesubiriwa kwa muda mrefu.

Kila mmoja, kwa nafasi na uwezo wake, ana wajibu wa kuchangia katika kulinda haki halali za Wapalestina, kuimarisha juhudi za kibinadamu na kupanua nafasi ya kupatikana kwa amani ya haki na ya kudumu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu awalinde wananchi wa Palestina, awarehemu waliopoteza maisha, awaponye waliojeruhiwa na awapunguzie machungu wote walioathirika. Amani na usalama viwafikie wananchi wa Palestina na watu wa mataifa yote.

Makala hii inatokana na tafisri ya hotuba ya Kiarabu kuhusu Palestina iliyotolewa tarehe 29 Oktoba 2026 katika Kongamano Kuhusu Palestina lililofanyika Hoteli ya Bahari Beach jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Wanadiplomasia, mabalozi (akiwemo balozi wa Palestina) na Masheikh.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanazuoni wa Kiislamu Tanzania (Hay-atul Ulamaa) akitoa hotuba ya ufunguzi wa mkutano wa kujadili Palestine uliondaliwa na Taasisi ya M A K. Masaajidi Ayadi Al kyer katika hoteli ya Sea Scape iliyopo Bahari beach kwa siku mbili, 29–30 Oktoba 2026

Haji Mrisho achaguliwa tena kuongoza TAMPRO



Jumuiya ya Wataalamu wa Kiislamu Tanzania (TAMPRO) imemchagua Haji Mrisho Rubibi kuwa Amir wake, katika uchaguzi wa viongozi uliofanyika Jumapili, Novemba 1, 2026, jijini Dar es Salaam.

Uchaguzi huo ulifanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa TAMPRO, uliondaliwa katika Hoteli ya Peacock, chini ya kaulimbiu “Uongozi Bora, Uadilifu na Maono ya Mbali.”

Matokeo hayo yametangazwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TAMPRO, Sheikh Suleiman Abdallah, ambaye pia amewataja viongozi wengine waliochaguliwa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Yahya Msonde amechaguliwa kuwa Naibu Amir, Dk. Fatuma Simba kuwa Katibu Mkuu na Hussein Meena kuwa Mweka Hazina.

Aidha, wajumbe 10 waliochaguliwa kuunda Kamati ya Utendaji ni Salum Awadh, Mohammed Kamilagwa, Hamisi Togwa, Hussein Mwamtuya, Sadiki Gogo, Dk. Said Jafari, Dk. Said Kuganda, Saleh Kassim, Mwanafumo Mohammed na Hadija Othman.

Akitoa salamu za shukrani baada ya uchaguzi, Haji Mrisho Rubibi aliwashukuru wanachama wa TAMPRO kwa ushirikiano, upendo na imani waliyoonyesha kwa viongozi waliomaliza muda wao, pamoja na timu mpya iliyochaguliwa.

Alisema TAMPRO ina wanachama wengi wenye uwezo na sifa za uongozi, hivyo uchaguzi unapaswa kuonekana kama kukabidhiana dhamana, huku wajibu wa kuijenga jumuiya ukiendelea kuwa wa wanachama wote.

Aliwataka wanachama kudumisha umoja, kusameheana na kushirikiana, huku wakiwaombea viongozi waliochaguliwa wapate hekima na busara katika kutekeleza majukumu yao.

“Bado tuna kazi kubwa na safari ndefu ya kuwatumikia Waislamu wa Tanzania. Kwa umoja na msaada wa Allah, tunaweza kufika mbali zaidi,” alisema.

Rubibi pia alimuomba Mwenyezi Mungu aibariki TAMPRO na kuiwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa manufaa ya jamii ya Waislamu nchini.



VISION 2050

JUMADA AL-AWWAL 23, 1448

HABARI NA
PANGANI, TANGA
Na mwandishi wetu

Shule za Al Hijra zajivunia kuzalisha wataalamu wa fani mbalimbali



Shule za Al Hijra Islamic, zinazomilikiwa na Taasisi ya Ansaar Muslim Youth Centre, zimeeleza kujivunia wahitimu wake wanaohudumu katika sekta mbalimbali nchini, wakiwemo askari polisi, walimu na wafanyabiashara.

Mafanikio hayo yalielezwa katika mahafali ya 14 ya kidato cha nne ya Al Hijra Islamic Secondary School, yaliyofanyika Novemba 1, 2026, eneo la Funguni, wilayani Pangani, mkoani Tanga.

Mahafali hayo yalihudhuriwa pia na wahitimu wa zamani wa shule hiyo, ambao sasa wanafanya kazi katika taaluma mbalimbali, huku wengine wakiendelea na masomo katika vyuo vikuu.

Akizungumza katika hafla hiyo, mmoja wa wahitimu hao, Hajj Huktuba Hajj, ambaye sasa ni askari polisi anayehudumu katika Dawati la Jinsia wilayani Pangani, aliwapongeza walimu kwa kazi ya kuwalea wanafunzi.

Aliwataka wahitimu wa kidato cha nne kudumisha maadili waliyofundishwa shuleni na kuwa mfano mzuri katika jamii.

Kwa upande wake, Aisha Msofe, aliyetambulishwa kuwa katibu wa mbunge wa Pangani, alizipongeza shule hizo kwa mchango wake katika elimu na kuahidi kusaidia juhudi za kuendeleza sekta hiyo. Shule ya msingi ya Al Hijra Islamic ilianzishwa Mei 29, 2001, ikitoa elimu kuanzia ngazi ya awali hadi darasa la saba, huku shule ya sekondari ikianzishwa Januari 1, 2011.

Shule hizo zimekuwa zikichanganya elimu ya kawaida na malezi ya Kiislamu yanayozingatia Qur'an na Sunna, kwa lengo la kuwajenga wanafunzi wenye maarifa, nidhamu na maadili mema.

Wanawake waandika historia mahafali ya TIA Zanzibar

Wanawake visiwani Zanzibar wameandika historia katika elimu ya juu baada ya kutawala orodha ya wahitimu wa mahafali ya kwanza ya Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kampasi ya Zanzibar, hatua inayoashiria mabadiliko ya mtazamo wa jamii kuhusu elimu ya mtoto wa kike.

Katika mahafali hayo yaliyofanyika Oktoba 28, 2026, wahitimu 188 waliotunukiwa vyeti na shahada, wanawake walikuwa 127 sawa na asilimia 68 huku wanaume wakiwa 61.

Mgeni rasmi, Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, alisema mafanikio hayo yanaonesha kupungua kwa changamoto zinazokwamisha wasichana kuendelea na elimu ya juu, akiwapongeza wazazi kwa uwekezaji wao katika elimu ya watoto bila ubaguzi wa kijinsia.

Waziri Omar aliwataka wahitimu kuzingatia uadilifu, utiifu wa sheria, ubunifu wa kiteknolojia na weledi ili waweze kushindana katika soko la ajira na kuchangia maendeleo ya taifa.

Mkuu wa Taasisi ya TIA, Prof. William Pallangyo, alisema jumla ya wahitimu 123 walitunukiwa shahada za uzamili, huku 65 wakitunukiwa vyeti vya ngazi mbalimbali. Alibainisha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wahitimu wa shahada za uzamili ni watumishi wa wizara na taasisi za umma Zanzibar.

Alisema kuwa uwepo wa kampasi hiyo umepunguza gharama za usafiri na malazi kwa wanafunzi waliokuwa wakilazimika kwenda Tanzania Bara kutafuta elimu hiyo.

Katika kuimarisha huduma, Serikali ya Zanzibar inajenga kampasi ya kudumu Makunduchi katika eneo la hekari 60 lililotolewa na Rais wa Zanzibar, Hussein Mwinyi ambapo utekelezaji wa awamu ya kwanza wenye thamani ya Sh15.9 bilioni umefikia asilimia 45.

Aidha, Prof. Palangyo alisema mradi huo unachochea uchumi wa eneo hilo, ambapo asilimia 70 ya vibarua ni vijana wa Makunduchi.

زكاة

NA
Na Baitulmaal Tanzania

JUKWAA LA ZAKA

Historia ya Baytulmaal na uhusiano wake na Zaka

Uislamu haukuja tu kujenga uhusiano wa mwanadamu na Mwenyezi Mungu kupitia ibada binafsi, bali pia kuweka misingi ya haki, mshikamano na uwajibikaji wa kijamii.
Miongoni mwa mifumo muhimu iliyowekwa na Uislamu ni Zaka, ambayo ni nguzo ya Uislamu na njia ya kusafisha mali na kuimarisha ustawi wa jamii.
Katika historia ya Kiislamu, Zaka haikuwa ibada ya mtu binafsi pekee, bali pia ilikuwa na mfumo wa ukusanyaji, usimamizi na ugawaji kwa watu wanaostahiki. Hapa ndipo tunapoelewa nafasi ya Baytulmaal kama taasisi ya kusimamia mali za umma na kuhakikisha zinatumika kwa mujibu wa Sharia.
Ili kuelewa Baytulmaal ya leo, ni muhimu kurejea historia ya Zaka katika kipindi cha Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), namna ilivyokusanywa na kugawiwa kwa walengwa, pamoja na maendeleo ya usimamizi wa mali za umma katika zama za Makhalifa Waongofu.

Baytulmaal: Maana ya kilugha na kisheria

Kilugha, neno Baytulmaal linatokana na maneno mawili ya Kiarabu: Bayt, lenye maana ya nyumba, na Al-Maal, linalomaanisha mali au utajiri. Kwa hiyo, Baytulmaal maana yake ni “nyumba ya mali”, yaani hazina au mfumo uliotumika kuhifadhi, kusimamia na kugawa mali za umma.

Kwa maana ya kisheria na kiutawala katika Uislamu, Baytulmaal ni mfumo au taasisi inayosimamia mali na rasilimali za umma, zinazokusanywa na kutumiwa kwa mujibu wa Sharia, huku haki za walengwa zikizingatiwa.

Katika historia ya Uislamu, mali zilizosimamiwa na Baytulmaal zilijumuisha Zaka na mapato mengine ya umma, yakiwemo Fay’ (mali zilizopatikana bila mapigano) na Kharaj (kodi ya ardhi iliyotozwa katika mazingira maalumu ya utawala wa Kiislamu), pamoja na aina nyingine za mapato yaliyotambuliwa kisheria.

Vyanzo tofauti, matumizi tofauti

Hata hivyo, kuna tofauti muhimu kati ya Zaka na mapato mengine ya Baytulmaal.

Zaka ina walengwa maalumu waliotajwa na Allah katika Surat At-Tawbah, aya ya 60. Baytulmaal, kwa upande mwingine, ni mfumo mpana wa usimamizi wa mali za umma.

Hii ina maana si kila mali inayosimamiwa na taasisi hiyo ina hukumu sawa na Zaka. Kwa hiyo, fedha za Baytulmaal haziwezi kutumiwa kwa madhumuni yoyote bila kuzingatia chanzo chake na masharti ya Sharia yanayohusika.

Kufaradhishwa kwa Zaka

Zaka ni miongoni mwa nguzo tano za Uislamu. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema”Uislamu umejengwa juu ya mambo matano...”

Katika Hadith hiyo, Mtume ametaja kushuhudia kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mtume Wake, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, kufunga Ramadhani na kuhiji kwa mwenye uwezo. [Bukhari na Muslim]. Hii inaonyesha kuwa Zaka si mchango wa hiari unaotegemea utashi wa mtu, bali ni ibada ya lazima pale masharti yake yanapotimia.

Hatua za ufaradhishwaji wa Zaka

Katika kipindi cha Makka, Qur’an ilisisitiza umuhimu wa kutoa mali, kuwasaidia maskini na kutambua haki za wahitaji. Aya nyingi zilihimiza utoaji na kukemea ubakhili.

Baada ya Hijra kwenda Madina, jamii ya Waislamu ilianza kujengwa ikiwa na taasisi na majukumu ya pamoja.

Katika kipindi hiki cha Madina, hukumu za Zaka zilifafanuliwa zaidi, zikiwemo viwango, aina za mali zinazopaswa kutolewa Zaka, masharti na walengwa wake.

Wanazuoni wengi wanaeleza kuwa mfumo wa Zaka ya lazima, wenye taratibu maalumu za ukusanyaji na viwango, uliimarishwa katika kipindi cha Madina, ingawa Qur’an ilikuwa imezungumzia utoaji wa mali tangu kipindi cha Makka.

Hivyo, ni muhimu kutofautisha wajibu wa kusaidia wahitaji, uliosisitizwa katika mafundisho ya awali, na mfumo wa Zaka ya lazima wenye masharti na taratibu maalumu.

Kuhusu ukusanyaji wa Zaka, Allah anasema:

“Chukua katika mali zao sadaka itakayowasafisha na kuwatakasa kwayo.” [Qur’an, 9:103].

Aya hii ina umuhimu mkubwa katika kuelewa historia ya Baytulmaal. Inamuamuru Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kuchukua sadaka katika mali za watu, hivyo kuonyesha kwamba Zaka ilikuwa na mfumo wa ukusanyaji na usimamizi, mbali na kuwa ibada binafsi.

Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa kila Mwislamu analazimika kuwasilisha Zaka yake kwa taasisi moja katika mazingira yote. Ukusanyaji na ulipaji wake hutegemea hukumu za Sharia na mamlaka husika.

Walengwa wa Zaka

Allah amebainisha makundi manane ya wanaostahiki Zaka katika Surat At-Tawbah, aya ya 60.

Mosi, mafukara; pili, maskini; tatu, wanaofanya kazi ya kukusanya na kusimamia Zaka; nne, wanaopewa Zaka ili nyoyo zao ziunganishwe; tano, wanaostahiki kusaidiwa katika kujikomboa kutoka utumwani; sita, wenye madeni wanaostahiki; saba, wanaostahiki katika njia ya Allah, kwa mujibu wa tafsiri na mipaka inayokubalika kifiqhi; na nane, wasafiri waliokwama na kuhitaji msaada.

Allah anahitimisha aya hiyo kwa kueleza kuwa mgawanyo huu ni wajibu uliowekwa na Yeye.

Hivyo, Zaka ina masharti maalumu ya kisheria kuhusu walengwa wake. Taasisi ya Baytulmaal inapaswa kuhakikisha fedha za Zaka zinatengwa na kutumiwa kwa kuzingatia masharti hayo.

وقف

MAKALA ZA WAQF

NA
Na Idara ya elimu Awqaf

Ipate Jannah kwa elfu moja, simu na fintech

Kwa muda mrefu, tumekuwa na dhana kwamba Waqf ni kwa matajiri pekee. Mwenye kiwanja, jengo au shamba kubwa ndiye anayeweza kufanya Waqf. Dhana hii imewafanya Waislamu wengi kujiona hawana uwezo wa kushiriki katika taasisi hii muhimu ya maendeleo ya Kiislamu.
Allah anasema: "Enyi mlioamini! Toeni katika vizuri mlivyovichuma..." [Qur'an 2:267].
Lakini zama zimebadilika. Kama teknolojia ya fedha kwa simu ilivyomrahisishia mkulima kufanya miamala bila kwenda benki, ndivyo teknolojia ya kifedha (Fintech) inavyoweza kumwezesha Muislamu wa kawaida kushiriki katika Waqf bila kuwa tajiri. Hii ndiyo fursa ya Waqf ya kidijitali.

Waqf ni kuzuia asili ya mali na kuelekeza manufaa yake kwenye shughuli za kheri. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), alipomshauri Umar bin al-Khattab kuhusu shamba lake la Khaybar, alimwelekeza kuhifadhi asili ya mali hiyo na kutoa mapato yake kama sadaka. Huo ndio msingi wa Waqfu.

Leo, asili ya Waqf haihitaji sana kuwa shamba; inaweza pia kuwa fedha inayokusanywa kutoka kwa watu wengi. Waislamu wengi wanatamani kuchangia shilingi 5,000 au 10,000, lakini hawajui wapi pa kupeleka fedha zao. Wengine wanahofia matumizi mabaya ya michango yao.

Allah anasema: "Hamtapata wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda." [Qur'an, 3:92].

Wakati tunalalamikia upungufu wa shule, vituo vya afya na ufadhili wa elimu, mara nyingi tunasubiri tajiri mmoja atoe mamilioni ya fedha. Tunasahau kwamba michango midogo ya watu wengi inaweza kujenga mtaji mkubwa na kuanzisha miradi yenye manufaa ya kudumu.

Tujifunze kutoka kwenye teknolojia ya fedha

Katika baadhi ya nchi, ikiwemo Malaysia, mifumo ya Waqf imeunganishwa na huduma za kifedha ili kurahisisha michango ya wananchi. Tanzania inaweza kutumia fursa hiyo kwa kuanzisha mifumo rafiki ya Waqf ya kidijitali.

Kwanza, taasisi zinazoaminika zinazosimamia Waqf zinaweza kushirikiana na watoa huduma za fedha kwa simu na benki kuanzisha namba maalumu za michango. Kupitia M-Pesa, Airtel Money, T-Pesa na mifumo mingine inayopatikana, kijana wa bodaboda anaweza kutoa buku moja, yaani shilingi 1,000, kila siku au kila wiki. Mfanyakazi anaweza kuchangia kiasi kilekile kila mwezi.

Pili, fedha hizo zisigawiwe zote mara moja. Zikusanywe na kuwekezwa katika miradi halali yenye mapato, kwa kuzingatia Sharia na masharti ya Waqf. Kwa mfano, mtaji unaweza kutumika kununua gari la biashara, kujenga maduka ya kupangisha au kuwekeza katika Sukuk zinazozingatia Sharia. Mapato yatakayopatikana yanaweza kusaidia kugharamia elimu, afya, mishahara ya walimu wa madrasa na mahitaji mengine yaliyokusudiwa.

Bila shaka, uwekezaji una hatari zake. Ndiyo maana miradi lazima ichaguliwe kwa uangalifu na kusimamiwa kitaalamu.

Tatu, uwazi ndiyo msingi wa uaminifu

Watu watachangia kwa moyo mkunjufu wakijua fedha zao zinakwenda wapi. Taasisi za Waqf zinapaswa kutoa taarifa za mapato, matumizi, uwekezaji na matokeo ya miradi. Mchangiaji apate ujumbe wa kuthibitisha mchango wake na taarifa za maendeleo ya Waqf. Ukaguzi huru wa hesabu nao ni muhimu kuzuia ubadhirifu na kulinda amana za wananchi.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema kuwa amali za mwanadamu hukatika anapokufa isipokuwa mambo matatu, mojawapo likiwa sadaka yenye kuendelea. [Muslim]. Waqf ni mojawapo ya njia za kuanzisha sadaka yenye manufaa yanayoendelea.

Kutoka kisima cha Uthman hadi buku la kidijitali

Uthman bin Affan (Allah amridhie) alitoa mchango mkubwa katika upatikanaji wa maji kwa Waislamu wa Madina kupitia kisima cha Ruma. Tukio hili linatukumbusha kwamba mali inaweza kuwa chanzo cha manufaa yanayovuka kizazi kimoja.

Katika zama zetu, tunaweza kuanzisha miradi ya Waqf kwa michango ya shilingi 1,000 kutoka kwa maelfu ya watu. Michango hiyo inaweza kusaidia kuchimba kisima, kujenga duka au kufadhili elimu ya mwanafunzi.

Hatuhitaji kusubiri kila kitu kiwe tayari ndipo tuanze. Tunahitaji taasisi zenye uaminifu, mifumo salama ya malipo na usimamizi unaozingatia Sharia na sheria za nchi.

Badala ya kuomba mtu mmoja atoe milioni 200 za kujenga msikiti, tunaweza kuwaalika watu 200,000 kuchangia shilingi 1,000 kila mmoja. Huo ni uwezo wa umoja unaowezeshwa na teknolojia.

Katika hesabu za Jannah, buku linaweza kuwa mwanzo wa mengi!

Allah anasema: "Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyochipua mashuke saba, katika kila shuke mna punje mia moja..." [Qur'an, 2:261].

Hatutakiwi kudharau mchango mdogo. Buku moja, likiwa sehemu ya Waqf uliosimamiwa vizuri, linaweza kusaidia kujenga taasisi yenye manufaa kwa vizazi vijavyo. Hatuwezi kuhesabu thawabu za Akhera kwa hesabu za fedha, lakini tunaweza kuanza leo kuwekeza katika sadaka yenye kuendelea.

Waqf si mali ya matajiri pekee. Kwa simu, uaminifu na 'buku moja', kila mmoja anaweza kuwa sehemu ya urithi wa kheri na kujityarishia njia ya peponi.

HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU



NA
Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

Sukuk za kijamii zatajwa suluhisho la changamoto Afrika

Matumizi ya hati fungani za Kiislamu zinazolenga maendeleo ya jamii (Social Sukuk) yametajwa kuwa njia mbadala ya kukusanya fedha za kugharamia miradi ya elimu, afya, ajira na kupunguza umaskini barani Afrika.

Mtaalamu wa usimamizi wa miradi ya Wakfu, Dkt. Salah Zahrani, amesema Sukuk hizo zinaweza kuvutia mitaji ya wawekezaji binafsi na kuelekeza fedha katika miradi yenye manufaa yanayoweza kupimwa.

Akizungumza na jarida la Financial Afrik, Oktoba 28, 2026, Dkt. Zahrani alisema tofauti na Sukuk za kawaida, Sukuk za kijamii hulenga kutatua matatizo maalumu ya jamii huku zikizingatia misingi ya Shariah.

Alieleza kuwa mfumo huo unaweza kuunganishwa na Wakfu wa fedha taslimu (Cash Waqf), unaowezesha watu wengi kuchangia kiasi kidogo cha fedha na kukusanya mtaji mkubwa wa kutekeleza miradi ya kijamii.

Kwa mujibu wake, Afrika ina fursa kubwa ya kutumia mfumo huo kutokana na mahitaji makubwa ya huduma za jamii, ufadhili wa biashara ndogo na ujumuishaji wa kifedha.

Changamoto tatu za bima rejeshi ya Kiislamu zatajwa

KUALA LUMPUR, Malaysia — Sekta ya bima rejeshi ya Kiislamu (Retakaful) inakabiliwa na changamoto za ushindani, mitaji na utaalamu, licha ya kukua kwa bima ya Kiislamu (Takaful) duniani.

Kwa mujibu wa ripoti ya Bodi ya Huduma za Fedha za Kiislamu (IFSB) ya 2026, mali za sekta ya Takaful zilizidi dola bilioni 71 kufikia robo ya tatu ya 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 13.9.

Katika makala yake iliyochapwa na Asia Insurance Review, Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Malaysian Re, Ahmad Noor Azhari Abdul Manaf, amesema ukuaji huo hauhakikishi kuongezeka kwa biashara ya Retakaful, ambao ni mfumo unaowezesha kampuni za Takaful kugawana hatari na mzigo wa fidia kwa kuzingatia Shariah.

Alisema kampuni hizo zinakabiliwa na ushindani kutoka kampuni za kawaida za bima rejeshi zenye mitaji na utaalamu mkubwa.

Hata hivyo, majanga ya tabianchi, gharama za matibabu na uhalifu wa kimtandao vinatoa fursa mpya za biashara.

Alisisitiza umuhimu wa kuimarisha mitaji, utaalamu wa kutathmini vihatarishi na uwezo wa kushughulikia madai ya fidia bila kukiuka Sharia.

Uzbekistan yatoa leseni ya kwanza ya benki ya Kiislamu

TASHKENT, Uzbekistan — Benki Kuu ya Uzbekistan imetoa leseni ya kwanza ya benki ya Kiislamu kwa Open Bank, Oktoba 23, 2026, kuruhusu huduma zinazozingatia Sharia, ikiwemo ufadhili wa biashara, ubia wa uwekezaji na ukodishaji mali.

Hatua hiyo imefuatia kupitishwa kwa sheria inayoruhusu benki kamili za Kiislamu na madirisha yake katika benki za kawaida.

Akizungumza kwenye kongamano jijini Samarkand, Gavana wa Benki Kuu, Timur Ishmetov, alisema serikali imeandaa mpango wa miaka mitano (2026–2030), wenye hatua 39 za kuendeleza sekta hiyo.

Pia, imeandaa rasimu ya sheria ya kuruhusu serikali na kampuni binafsi kutoa hati fungani za Kiislamu (Sukuk).

Tayari taasisi 11 za fedha ndogo zinatoa huduma za Kiislamu nchini humo.

Uzbekistan inalenga kuvutia uwekezaji wa ziada wa dola bilioni moja na kuanzisha benki mbili kamili za Kiislamu ifikapo 2030.

UNDP yasisitiza mchango wa huduma fedha za Kiislamu

GENEVA, Uswisi — Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP) limesisitiza umuhimu wa kutumia mifumo ya fedha za Kiislamu kugharamia miradi ya maendeleo, kupunguza umaskini na kuwawezesha wananchi kujitegemea kiuchumi.

Akizungumza katika mkutano wa kimataifa wa ufadhili wa maendeleo wa AidEx Geneva 2026, mtaalamu wa fedha za Kiislamu wa UNDP, Muniruddeen Lallmahomood, amesema mifumo hiyo ina uwezo mkubwa wa kuvutia mitaji kwa ajili ya maendeleo endelevu.

Alisema kuchanganya huduma za kibiashara za fedha za Kiislamu na mifumo ya kijamii, ikiwemo Zaka na Wakfu, kunaweza kuongeza fedha za kugharamia miradi ya elimu, afya, kilimo, nyumba nafuu na nishati jadidifu.

Kwa mujibu wa UNDP, mifumo hiyo inaweza kusaidia jamii maskini kuondokana na utegemezi wa misaada na kujenga uwezo wa kujitegemea kiuchumi.

NA UKHTI FATIMA



Mwanafunzi mjasiriamali: tamu, chungu na visa vya wateja

Ukiingia katika vyuo vikuu vya Tanzania, unaweza kudhani baadhi ya wanafunzi wanasomea digrii mbili kwa wakati mmoja: ile waliyoandikishwa chuoni na nyingine ya biashara!

Kuna wanaouza nguo, viatu, mikoba, vipodozi na pafyumu. Wengine wanauza simu, kompyuta mpakato na vifaa vya kielektroniki. Wenye mitaji mikubwa wanaendesha biashara za chakula, vitafunwa na vinywaji.

Kwa wengine, chumba cha hosteli kimegeuka ghala, simu imekuwa ofisi na WhatsApp ni duka lisilofungwa.

Biashara hizi zinawasaidia wanafunzi kujiongezea kipato, kupunguza utegemezi kwa wazazi na kujifunza ujasiriamali kwa vitendo. Lakini nyuma ya faida kuna mambo yanayoweza kumfanya mwanafunzi acheke leo na kulia kesho.

Jambo zuri ni kwamba biashara nyingi hazihitaji duka. Unaweza kutangaza bidhaa Instagram au WhatsApp, kupokea oda na kumfikishia mteja bidhaa alipo.

Na wateja si wanafunzi pekee. Hata walimu ni wateja! Mhadhiri anayekufundisha uchumi darasani anaweza kuwa mteja wako wa pafyumu, viatu au kompyuta. Lakini usije ukadhani akishanunua bidhaa zako, basi na alama za mtihani zitaongezeka!

Kwa biashara za chakula, soko linaweza kuwa zuri zaidi. Wanafunzi wanaweza kuacha kununua nguo mpya, lakini hawawezi kuacha kula. Hata hivyo, biashara hiyo inahitaji muda, usafi na usimamizi makini.

Katika mazingira haya, mtaji si fedha pekee. Urafiki na uwezo wa kuwasiliana vizuri na watu ni mali muhimu.

Mwanafunzi mwenye marafiki wengi anaweza kuuza bidhaa kwa urahisi zaidi. Mteja mmoja aliyeridhika anaweza kuleta wengine watano. Lakini pia mteja mmoja aliyedanganywa anaweza kuharibu jina lako kwenye vikundi vya WhatsApp!

Ndiyo maana uaminifu, ubora wa bidhaa, bei nzuri na kutimiza ahadi ni muhimu kuliko umaarufu.

Uzuri wa biashara chuoni ni kwamba unapata fedha huku ukijifunza mambo ambayo wakati mwingine hayafundishwi darasani. Unajifunza kupanga bei, kujadiliana na wateja, kutunza hesabu na kukabiliana na ushindani.

Fedha unazopata zinaweza kukusaidia kununua vifaa vya masomo, chakula na kugharamia usafiri bila kumtegemea mzazi kwa kila kitu.

Biashara pia inaweza kukujengea kujiamini, nidhamu ya fedha na mtandao wa wateja ambao utaendelea kukusaidia hata baada ya kuhitimu. Wengine wanaweza kuondoka chuoni wakiwa tayari wamejiajiri.

Lakini si kila kinachong'aa ni dhahabu.

Kuna mwanafunzi ambaye hata mhadhiri akifundisha jambo muhimu, akili yake ipo kwenye oda ya viatu. Simu ikiita, anatoka darasani kwenda kumpokea mteja. Mwisho wa muhula, biashara inaendelea vizuri lakini matokeo ya mtihani yanatia huruma.

Kuchanganya biashara na masomo kunahitaji nidhamu. Kupokea oda, kutafuta bidhaa na kusambaza mizigo kunaweza kumchosha mwanafunzi, kumnyima usingizi na muda wa kujisomea.

Halafu kuna ugonjwa mwingine wa biashara za chuoni: mikopo!

Shoga yako kipenzi anakuomba gauni kwa mkopo. Unampa kwa sababu mmezoeana. Wiki mbili zinapita, mwezi unapita, kila ukimuuliza anakwambia, "Wewe si unajua hali yangu?"

Siku unapoamua kudai kwa msisitizo, urafiki unaanza kupasuka. Mlikuwa marafiki wa kula sahani moja, sasa mnapishana koridoni kama hamjuani!

Mikopo inaweza kumaliza mtaji na kuharibu mahusiano. Hata hivyo, si kila mkopo ni mbaya; tatizo ni kuuza bila makubaliano ya wazi na uhakika wa malipo.

Hatari nyingine ni kutumia mtaji kwa tamaa binafsi. Umeuza pafyumu ukapata faida, mara unaona viatu vizuri Instagram. Badala ya kurudisha fedha kwenye biashara, unanunua viatu. Kesho unaona mkoba unaokuvutia, unanunua tena.

Hujafika mwisho wa muhula, mtaji umekwisha, lakini kabati limejaa nguo na viatu!

Kwa wanafunzi wa kike, kuna changamoto nyingine inayohitaji tahadhari.

Si kila mwanaume anayekuja kununua bidhaa ana nia ya biashara pekee. Wengine hutumia oda na mazungumzo ya kibiashara kama kisingizio cha kujenga ukaribu usiofaa.

Anaanza kuulizia bei ya pafyumu. Kesho anaomba picha zaidi za bidhaa. Keshokutwa mazungumzo yanageuka kuwa, "Mbona leo hujanisalimia?"

Hatimaye, biashara inakuwa mlango wa mahusiano yanayoweza kuvuka mipaka ya dini na maadili. Hata hivyo, hii haimaanishi kila mteja mwanaume ana nia mbaya. Mwanafunzi anapaswa kujenga mazingira ya biashara yenye mipaka, kuheshimu wateja na kujilinda dhidi ya ushawishi usiofaa.

Biashara pia ina misimu yake. Wakati wa likizo, wanafunzi wanaporudi nyumbani, hakuna biashara, na kama una bidhaa zinaweza kuharibika au kukosa wanunuzi, hivyo kusababisha hasara.

Kwa hiyo, kabla ya kuanza biashara, mwanafunzi anahitaji kujiuliza: Je, biashara hii inalingana na ratiba yangu? Nina mtaji wa kutosha? Nitawezaje kuitenganisha na matumizi binafsi?

Ni vizuri kuwa na kumbukumbu za mapato na matumizi, kupunguza mikopo na kutenga muda maalumu wa biashara. Wakati wa mitihani, vitabu vinapaswa kupewa kipaumbele kuliko oda.

Vyuo navyo vinaweza kusaidia kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuweka mazingira mazuri ya biashara halali bila kuathiri masomo.

Mahafali ya Forest Hill: Wahitimu waaswa nidhamu, maadili mema

Wahitimu wa Shule ya Sekondari Forest Hill mkoani Morogoro wametakiwa kutumia elimu na malezi waliyoyapata kuwa mfano wa kuigwa katika jamii kwa kuzingatia nidhamu, maadili mema na kudumisha amani.

Wito huo umetolewa na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Khalid Matengo, aliyemwakilisha Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdul Aziz Abood, katika mahafali ya Kidato cha Nne ya shule hiyo inayomilikiwa na The Islamic Foundation.

Akizungumza kwa niaba ya mbunge huyo, Matengo aliipongeza The Islamic Foundation kwa mchango wake katika elimu na malezi, akisema Forest Hill ina historia ya kuzalisha viongozi, wafanyabiashara, madaktari, wahandisi na wataalamu wa kada mbalimbali.

Aliwataka wahitimu kuendeleza mafanikio ya watangulizi wao na kutumia maarifa waliyopata kuchangia maendeleo ya taifa.

“Tunawapenda sana wahitimu wote na tunawaombea mafanikio makubwa katika maisha yao. Tunawaomba muendeleze mafanikio ya watangulizi wenu kwa kutambua kuwa mnapita katika njia ambayo wengine wamepita na kufanya mambo makubwa kwa taifa,” alisema.

Pia, aliwapongeza wazazi kwa kuchagua shule hiyo, huku akiwakumbusha kuwa malezi ya watoto ni jukumu la pamoja kati ya familia, shule na jamii.

Alisema changamoto ya kuporomoka kwa maadili inahitaji ushirikiano katika kuwajenga vijana wenye elimu, nidhamu na tabia njema. Aidha, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya athari za mvua za El Niño kwa kufuata maelekezo ya mamlaka husika.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Kidato cha Nne, Yahya Hamidu, alisema shule ina matarajio makubwa kwa wahitimu kutokana na maandalizi ya kitaaluma na mafunzo ya dini na maadili waliyopata.

Alisema wanafunzi wamefundishwa misingi ya akhlaki kwa kufuata mafundisho ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), hivyo wanatarajiwa kuwa mfano mwema katika jamii.

Aliwahimiza wazazi kuendelea kusimamia malezi ya watoto wao hata baada ya kuhitimu, huku akieleza kuwa Forest Hill inatoa elimu ya kawaida na ya dini inayowaandaa vijana kukabiliana na changamoto za maisha.

Nao baadhi ya wazazi walieleza kuridhishwa na elimu, malezi na mazingira salama ya shule hiyo, wakisema yanachangia ukuaji wa watoto kitaaluma na kimaadili.

Katika risala yao, wahitimu waliishukuru The Islamic Foundation kwa kuendeleza shule hiyo na kuomba taasisi hiyo kufikiria kuanzisha chuo cha ufundi ili kuwapa vijana fursa zaidi za kujifunza ujuzi wa kujiajiri.





MATUKIO KATIKA PICHA
Na abdulrahman Omar
0655 763 580

Mahafali ya Kidato cha Nne ya Shule ya Sekondari ya Forest Hill, mjini Morogoro











خطبة الجمعة

IMEANDALIWA
Na Barnabas Mkwayu
0766 364 354

MIMBARI ZETU

KUTOKA

Masjid Al-Haram **(Makka)**

Masjid Nabawi **(Madina)**



450266447

MIMBARI ZETU

خطبة الجمعة

MSIKITI MTAKATIFU, MAKKA

IMAMU NA KHATIBU SHEIKH DKT. SALEH BIN ABDULLAH BIN HUMAID



Imamu Makka ataja siri 3 za kupata utulivu wa moyo

MAKKA, Saudi Arabia — Imamu na Khatibu wa Msikiti Mkuu wa Makka, Sheikh Dkt. Saleh bin Abdullah bin Humaid, amesema utulivu wa kweli wa moyo na furaha ya maisha havitegemei wingi wa mali, bali uimara wa imani, kumtegemea Allah na kuridhika na maamuzi Yake.

Katika khutba ya Ijumaa, Oktoba 23, 2026, Sheikh Bin Humaid alisema baadhi ya watu huishi kwa utulivu na kuridhika licha ya changamoto zinazowakabili, huku wengine wakiwa na mali na starehe nyingi lakini wakiendelea kukabiliwa na huzuni, wasiwasi na kutoridhika.

Alieleza kuwa tofauti hiyo inahusiana na kile kinachoitwa halawatuliman, yaani utamu wa imani, ambao humwezesha muumini kupata utulivu wa ndani na kustahimili misukosuko ya maisha.

Kwa mujibu wa khatibu huyo, utamu wa imani hupatikana kwa kuridhika na Allah kuwa Mola, Uislamu kuwa dini na Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) kuwa Mtume na Mjumbe wa Allah. Alisema kuridhika na Allah kunamaanisha kutambua kuwa Yeye ndiye Muumba, Mruzuku na Msimamizi wa mambo yote, huku kuridhika na Uislamu kukimaanisha kuukubali kama mwongozo wa maisha; na kuridhika na Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) kunamtaka Muislamu kufuata mafundisho, mwenendo na Sunna zake. Sheikh Bin Humaid alisema Muumini mwenye imani thabiti hushukuru anapopewa neema, huwa na subira anapokosa anachokitamani na hukimbilia kutubu anapofanya dhambi.


Alionya kuwa kudhoofika kwa imani kunaweza kumfanya mtu kuwa mwenye wasiwasi, kukata tamaa na kutawaliwa na ubinafsi, hali inayoweza kuathiri pia uhusiano wake na wengine.

Aliwahimiza Waislamu kuimarisha uchamungu, kufanya ibada kwa ikhlasi, kushikamana na Sunna na kujitahidi kutenda mema.

Alisisitiza kuwa furaha ya kweli inapaswa kutafutwa katika uhusiano wa mtu na Allah, badala ya kutegemea mafanikio ya mali na starehe za dunia pekee.

MSIKITI WA MTUME, MADINA

IMAM NA KHATIBU SHEIKH DKT. ALI BIN ABDULRAHMAN AL-HUDHAIFI



Umoja wa Waislamu ujengwe katika Tauhidi, Qur'an na Sunna

MADINA, Saudi Arabia — Imamu na Khatibu wa Msikiti wa Mtume mjini Madina, Sheikh Dkt. Ali bin Abdulrahman Al-Hudhaifi, amewataka Waislamu kuimarisha umoja wao kwa kushikamana na Tauhidi, Qur'an na Sunna, akisisitiza kuwa kutamka shahada mbili pekee hakutoshi bila kuzitekeleza katika maisha.

Katika khutba ya Ijumaa, Oktoba 23, 2026, Sheikh Al-Hudhaifi alisema shahada ya kushuhudia kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mtume Wake ndiyo msingi wa imani ya Kiislamu.

Alieleza kuwa shahada ya kwanza inamtaka Muislamu kuelekeza ibada zote kwa Allah pekee, bila kumshirikisha na chochote, huku shahada ya pili ikimtaka kumtii Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), kuamini aliyoyafundisha na kufuata Sunna zake.

Khatibu huyo alisema Waislamu wanapaswa kuungana katika matendo kama walivyoungana katika kutamka shahada hizo, kwa kuimarisha udugu, kusaidiana na kuepuka mifarakano.

Akizungumzia umuhimu wa Tauhidi, Sheikh Al-Hudhaifi alisema ujumbe wa msingi wa Mitume wote ulikuwa kuwaelekeza watu kumwabudu Allah pekee na kujiepusha na shirki.

Alisisitiza pia umuhimu wa kumtambua Allah kupitia Majina na Sifa Zake zilizotajwa katika Qur'an na Sunna, kwa kufuata mafundisho ya Mtume na Maswahaba zake.

Kwa mujibu wa khatibu huyo, Waislamu wana mambo muhimu yanayowaunganisha, yakiwamo itikadi, lugha ya Kiarabu inayotumika katika ibada, historia ya ujumbe wa Mitume na Kibla kimoja.

Alitumia aya ya 103 ya Suratu Aal Imran inayowaamrisha Waumini kushikamana na kamba ya Allah kwa pamoja na kutofarakana.

Sheikh Al-Hudhaifi alisema changamoto zinazowakabili Waislamu zinahitaji ushirikiano, kusaidiana na kuhurumiana, badala ya mifarakano inayodhoofisha nguvu za Umma.

JUMADA AL-AWWAL 23, 1448

KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

Kwa mwenendo huu, bado tuna safari ndefu ya malezi

“Tunaomba Watanzania wote mtusamehe. Tumeonesha wazazi kwamba hawatulei vizuri pamoja na walimu wetu. Kwa hiyo, ningependa mtusamehe,... naomba msamaha kwa walimu wetu kwa sababu tumefanya utovu wa nidhamu. Tunaomba msamaha kwa Serikali na shule yetu.”

Hizo ni kauli za baadhi ya wahitimu wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Aboud Jumbe iliyopo Kigamboni jijini Dar es Salaam, walioomba radhi kwa walimu, wazazi, Serikali na Watanzania kufuatia kusambaa kwa video inayowaonesha wakitumia lugha isiyozingatia maadili kwenye mitandao ya kijamii.

Kufuatia tukio hilo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dkt. Dorothy Gwajima amekemea matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii kwa baadhi ya wanafunzi wa kike, akivitaja vitendo hivyo kuwa ni vya kijinga.

Kwanza, tunawapongeza wanafunzi hao kwa kutambua makosa yao na kuomba msamaha. Hata hivyo, ni muhimu kwao kuthibitisha kwa vitendo kuwa wamejifunza kutokana na makosa hayo kwa kubadili mwenendo wao, kujiepusha na tabia zisizofaa na kuzingatia maadili, uwajibikaji na matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii.

Kukiri kosa ni hatua ya kwanza, lakini uwajibikaji wa kweli huonekana kupitia mabadiliko ya tabia. Tukio hili linapaswa kuwa funzo kwa wazazi, walimu na jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kuimarisha malezi ya vijana, hasa katika kipindi hiki cha matumizi makubwa ya teknolojia.

Tuna wajibu wa kuwasaidia vijana kuelewa kuwa mafanikio ya elimu hayapimwi kwa ufaulu pekee, bali pia kwa kuwa na nidhamu, kuonesha heshima na kuwajibika katika jamii.

Katika surat Luqman [Qur’an, 31:13–19], zimeelezwa nasaha za Luqman kwa mwanawe kuhusu kumwabudu Mwenyezi Mungu, kusimamisha sala, kuhimiza mema, kukataza maovu na kujiepusha na kiburi.

Nasaha hizi zinasisitiza umuhimu wa kuanza malezi mapema na kuyajenga katika misingi imara ya imani, maadili mema na kuwaheshimu wengine. Vijana na watoto wanahitaji kupewa ushauri na mwongozo katika maisha yao ya kila siku, badala ya kusubiri wafanye makosa hadharani ndipo waanze kufundishwa maadili.

Ni muhimu pia kuchunguza sababu zinazochangia mwenendo usiofaa miongoni mwa watoto na vijana na kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia kujirudia kwa matukio kama hayo. Wazazi na walezi wana wajibu wa kufuatilia mienendo ya vijana wao na kuwaelimisha kuhusu madhara ya maamuzi wanayofanya, hususan katika matumizi ya mitandao ya kijamii.

Aidha, walimu wanapaswa kuimarisha elimu ya maadili shuleni, huku Serikali na wadau wengine wakiendeleza kampeni za kuhamasisha matumizi salama na yenye uwajibikaji ya teknolojia.

Ili kujenga jamii yenye vijana wenye nidhamu, maadili na uwajibikaji, ni lazima tuimarishe misingi ya malezi bora kuanzia ngazi ya familia hadi shuleni sambamba na kukuza ushirikiano miongoni mwa wanajamii. Tusipofanya hivyo tutaendelea kushughulikia matokeo ya makosa badala ya kuzuia sababu zake.

VISION 2050

جُمادى الأول

DARASA LA WIKI



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

Hivi ndivyo unavyopaswa kuoga janaba

Uislamu umeweka sharia mbalimbali zinazohusiana na afya na usafi wa mwili. Busara na hekima iliyomo katika baadhi ya sharia hizo imezidi kufahamika katika nyakati za sasa. Miongoni mwa sharia hizo ni kuoga janaba, ambapo baadhi ya ibada hutekelezwa baada ya kujitwaharisha kwa mujibu wa sharia. Ni wajibu kwa kila Muislamu kujifunza hukumu zinazohusiana na kuoga janaba ili aweze kuzitekeleza kwa usahihi. Aidha, Muislamu anapaswa kuuliza mambo asiyoyajua, kama Allah Mtukufu alivyosema: "Basi waulizeni wenye kujua ikiwa nyinyi hamjui" [Qur'an, 16:43]. Kuoga janaba ni faradhi inayopaswa kuzingatiwa na kila Muislamu anapokuwa katika hali inayolazimu kufanya hivyo. Sasa basi, ni ipi njia sahihi ya kuoga janaba kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu?
Je, kutawadha ni sharti kabla ya kuoga janaba? Na je, kuoga janaba ni wajibu hata pale tendo la ndoa linapofanyika bila ya kutokwa na manii (mbegu za uzazi)?

Maana na hekima ya kuoga janaba

Wanazuoni wameeleza kuwa kuoga janaba ni kuosha mwili mzima bila kuacha sehemu yoyote, kwa nia ya kujitwaharisha ili kutekeleza ibada. Allah Mtukufu anasema: "Na mkiwa na janaba, basi ogeni (jitwaharisheni)." [Qur'an, 5:6].

Pia Allah anasema: "Enyi mlioamini! Msikaribie swala hali ya kuwa mmelewa, mpaka myajue mnayoyasema, wala mkiwa na janaba, isipokuwa mnapokuwa safarini, mpaka muoge josho..." [Qur'an, 4:43].

Mambo yanayosababisha janaba

Mosi, kutoka manii kwa mwanaume au mwanamke

Mtu akiwa macho, kutoka kwa manii kunakotokana na hisia za ashiki kunamwajibisha kuoga janaba. Hata hivyo, manii yakitoka bila ya hisia, kwa mfano kutokana na ugonjwa au sababu nyingine, hali hiyo haiwajibishi kuoga janaba.

Aidha, mtu anapoamka usingizini na kukuta athari ya manii mwilini au kwenye nguo zake, analazimika kuoga janaba hata kama hakumbuki kuota ndoto inayohusiana na tendo la ndoa.

Hukumu hii inatokana na riwaya ya Mama Aisha (Allah amuwie radhi), aliyesimulia kuwa Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) amesema: "Mwanamke akiota na akaona maji (manii), basi aoge janaba." Hata hivyo, mtu akiota ndoto bila kuona athari ya manii halazimiki kuoga janaba.

Pili, kufanya tendo la ndoa

Kuoga janaba ni wajibu baada ya kufanya tendo la ndoa, hata kama hakuna manii yaliyotoka. Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Tupu mbili zinapokutana, kuoga janaba ni wajibu" [Muslim]. Hivyo, mwanaume na mwanamke wanawajibika kuoga janaba baada ya kujamiiana hata kama hawakutokwa na manii.

Tatu, kusilimu

Kuhusu mtu anayeingia katika Uislamu, wanazuoni wana mitazamo tofauti kuhusu hukumu ya kuoga janaba.

Baadhi yao wanasema kuwa ni wajibu kwa mtu aliyesilimu kuoga, wakitegemea riwaya zinazoeleza kuwa Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) aliwaamuru baadhi ya watu waliosilimu kuoga. Hata hivyo, wanazuoni wengine wanaona kuwa kuoga katika hali hiyo ni sunna na si wajibu.

Nne, kufa

Maiti wa Kiislamu anapaswa kuoshwa kabla ya kuzikwa, isipokuwa shahidi (aliyekufa vitani), ambaye ana hukumu maalumu katika Uislamu. Mtume ameelekeza maiti aoshwe kwa maji na majani ya mkunazi, kisha avishwe sanda.

Tano, kumalizika kwa hedhi au nifasi

Mwanamke anapomaliza hedhi au nifasi na kutwaharika analazimika kuoga ili kurejea katika hali ya twahara inayomwezesha kutekeleza ibada zinazohitaji twahara, ikiwemo sala. Hukumu hii imeelezwa katika Qur'an na hadith za Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie).

Namna sahihi ya kuoga janaba

Kuna namna mbili za kuoga janaba.

Kwanza, kuoga kwa kiwango cha lazima. Hii ni njia ya kuoga inayotosheleza kuondoa janaba na inahusisha mambo mawili: kuweka nia moyoni ya kujitwaharisha kutokana na janaba na kueneza maji katika mwili mzima bila kuacha sehemu yoyote.

Kwa njia hii, mtu hutwaharika bila ya kulazimika kutawadha kando, kwa kuwa udhu unaweza kujumuishwa katika kuoga janaba.

Pili, kuoga kwa ukamilifu. Hii ndiyo njia bora ya kuoga janaba, inayofuata utaratibu uliofundishwa na Mtume (rehema na amani zimshukie). Muogaji huanza kwa kuweka nia moyoni, kisha huosha mikono na sehemu za siri kabla ya kutawadha kama anavyotawadha kwa ajili ya sala.

Baada ya hapo, humimina maji kichwani mara tatu, akihakikisha yanafika kwenye mashina ya nywele. Kisha huosha upande wa kulia wa mwili, ukifuatiwa na upande wa kushoto, huku akihakikisha maji yanafika sehemu zote za mwili.

Katika hatua zote za kuoga janaba, ni muhimu kuhakikisha maji yanafika sehemu zote za mwili, zikiwemo sehemu zilizojificha kama kwapani, kitovuni na nyuma ya magoti. Aidha, mtu aliyevaa pete au saa anapaswa kuzisogeza ili kuhakikisha maji yanafika kwenye ngozi iliyo chini yake.

Kwa mwanamke aliyemaliza hedhi au nifasi, ni muhimu kuhakikisha maji yanafika kwenye mashina ya nywele. Kufumua nywele zilizosukwa si lazima ikiwa maji yanafika kwenye mashina yake.

NA
Na Said Rajab
0783 650 803

Matumizi ya Akili Unde kwa mtazamo wa Kiislamu



Katika toleo lililopita, tulijadili changamoto nne za kiroho zinazotokana na matumizi ya Akili Unde (AI). Tulieleza kuwa ni haramu kubuni fat–wa, hadith, maoni ya wanazuoni na hukumu za kidini za uongo. Tulisisitiza pia kuwa kuunda maimamu au wanazuoni bandia na kutumia vibaya hisia za kidini za watu kupitia Akili Unde ni vitendo visivyokubalika na vilivyoharamishwa.

Aidha, tuliwahimiza Waislamu kuthibitisha taarifa zote za kidini kwa kuwahusisha wanazuoni halisi na kutokubali maudhui ya kidini yanayotolewa na Akili Unde bila kuyathibitisha. Sasa tuendelee na sehemu inayofuata...

A tatu za akili unde

Wanazuoni wa Kiislamu wameweka mfumo wa kutathmini matumizi ya teknolojia ya Akili Unde (AI). Ili kuhakikisha matumizi yake yanaendana na maadili ya Kiislamu, mfumo huo unazingatia vigezo vitatu vya A, ambavyo ni Agency (Akili), Accountability (Amana na uwajibikaji) na Authenticity (Ukweli na uhalisia). Hebu tuvitazame kimoja baada ya kingine.

Agency (Akili)

Uamuzi na usimamizi wa kimaadili lazima vibaki mikononi mwa binadamu. Akili Unde ni chombo cha kusaidia tu; haiwezi kuchukua nafasi ya hukumu ya kibinadamu, dhamiri au uwezo wa kufanya maamuzi.

Kwa hiyo, binadamu lazima aendelee kuongoza matumizi ya Akili Unde.

Accountability (Amana na uwajibikaji)

Uwajibikaji hauwezi kuhamishiwa kwenye mashine. Jukumu la matokeo ya matumizi ya Akili Unde linabaki kwa binadamu. Ikiwa mtu atatumia AI kusababisha madhara, atawajibika kwa matendo yake mbele ya Mwenyezi Mungu na hapaswi kuilaumu algoriti.

Authenticity (Ukweli na uhalisia)

Ni muhimu kukataa aina zote za udanganyifu wa kidijitali. Maudhui yanayotolewa na Akili Unde yanapaswa kuwa sahihi, ya kweli na yaliyothibitishwa.

Kutumia Akili Unde kwa udanganyifu ni kwenda kinyume na msingi muhimu wa maadili ya Kiislamu wa Sidq, yaani kusema na kutenda kwa ukweli.

Wajibu wa wasanifu wa programu za Akili Unde

Qur'an inasema: "Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni kuzirudisha amana kwa wenyewe." [Qur'an, 4:58]. Waislamu wanaofanya kazi katika sekta ya Akili Unde (AI), wakiwamo wahandisi wa programu, wanasayansi wa data na watafiti wa AI wana jukumu maalumu la kulinda amana hiyo.

Wasanifu Waislamu wa programu za AI wanapaswa kuhakikisha kuwa mifumo wanayounda ina vichujio vinavyozingatia misingi ya halali, inazuia taarifa potofu, haizalishi maudhui yanayokinzana na Uislamu, na inazuia udanganyifu pamoja na madhara. Huu si wajibu wa kawaida tu bali ni amana inayopaswa kutunzwa.

VISION 2050

جُمادى أول

NASAHA ZA WIKI

0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

Mambo muhimu yasiyofahamika kuhusu sadaka

Kwa lugha rahisi na nyepesi, sadaka ni kutoa mali au fedha, au kutenda jambo lolote jema kwa nia ya kumridhisha Mwenyezi Mungu. Hii ina maana kwamba sadaka haijumuishi utoaji wa fedha pekee, bali pia matendo yote mema yenye manufaa kwa mtu binafsi na jamii kwa ujumla.

Miongoni mwa matendo yanayohesabiwa kuwa sadaka ni kumtabasamia ndugu yako. Tabasamu la dhati linaweza kumfariji mtu, kumtia moyo na kumletea furaha, huku likichangia kuimarisha upendo na mshikamano katika jamii.

Vilevile, kusema maneno mazuri ni miongoni mwa matendo mema yanayohimizwa katika Uislamu. Maneno mazuri yana mchango mkubwa katika kudumisha amani, kuimarisha uhusiano baina ya watu na kumtia moyo mtu anayekabiliwa na changamoto mbalimbali.

Hivyo, kila mtu anaweza kutenda wema kupitia kauli na matendo yake bila kutumia fedha. Kuondoa kikwazo barabarani pia ni miongoni mwa matendo yanayohesabiwa kuwa sadaka.

Kuondoa mwiba, jiwe au kitu kingine kinachoweza kuhatarisha usalama wa wapita njia ni ishara ya kujali maisha na usalama wa wengine. Ingawa jambo hilo linaweza kuonekana dogo, linaweza kumkinga mtu dhidi ya ajali au madhara makubwa.

Aidha, kumsaidia mtu mwenye uhitaji, iwe kwa kumbebea mzigo, kumwelekeza njia au kumpatia mahitaji muhimu ni miongoni mwa matendo mema yenye thamani kubwa.

Kadhalika, kumpatia mtu mwenye uhitaji chakula au maji ni miongoni mwa matendo mema yenye thamani kubwa, hasa ikizingatiwa kuwa mahitaji hayo ni muhimu kwa ustawi na uhai wa binadamu.

Katika baadhi ya jamii, upatikanaji wa maji safi na salama bado ni changamoto, hali inayowalazimu wananchi kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo muhimu. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ametaja fadhila na umuhimu wa kuwasaidia watu wenye uhitaji.

Mtume amesema: “Muislamu yeyote atakayemvisha nguo Muislamu mwenzake, Allah atamvisha nguo za kijani zilizo Peponi. Muislamu yeyote atakayemlisha Muislamu mwenzake mwenye njaa, Allah atamlisha kutokana na matunda ya Peponi; na Muislamu yeyote atakayemnywesha Muislamu mwenzake mwenye kiu, Allah atamnywesha Siku ya Kiyama kutokana na kinywaji kilichofungwa (Rahiq Al–Makhtum).” [Tirmidhi].

Ndugu yangu Muislamu, usidharau kiasi kidogo cha maji unachoweza kutoa, kwani kinaweza kuwa msaada mkubwa kwa watu wanaokabiliwa na ukame na umasikini.

Kuwapatia watu wenye uhitaji maji, chakula, mavazi au fedha ni miongoni mwa matendo mema yanayosaidia kupunguza makali ya maisha na kuwawezesha kukidhi mahitaji yao ya msingi.

Aidha, kumfundisha mtu elimu yenye manufaa, kumwelekeza katika njia sahihi na kumsaidia kuelewa mambo muhimu ni matendo mema yanayogusa maisha ya watu wengi katika jamii. Kupatanisha watu waliogombana pia ni sadaka inayosaidia kurejesha amani na kuimarisha udugu.

Kiujumla, kila mtu ana nafasi ya kutenda wema kulingana na uwezo wake. Kwa mantiki hiyo, Muislamu hana sababu ya kukwepa ibada ya sadaka, kwani inajumuisha mali, kauli, matendo na kuzuia madhara kwa watu.

Jambo muhimu ni kuwa na nia njema, kutenda kwa ikhlas na kuepuka ria (kujionesha) au kumdhalilisha anayepokea msaada. Kumsaidia mwenye shida kwa kumpa ushauri, maelekezo au kumtahadharisha dhidi ya jambo baya pia kunazingatiwa kuwa ni sadaka.

Ukishindwa kutoa msaada, basi epuka kuwaudhi watu kwa mikono yako, ulimi wako na macho yako, kwani kujiepusha na kuwaudhi watu ni miongoni mwa mambo yanayomkurubisha mja kwa Allah.

Ndugu yangu Muislamu, usisubiri uwe tajiri ndipo utoe sadaka. Anza kwa kile ulichonacho, hata kama ni tabasamu, neno jema au msaada mdogo kwa mtu mwenye uhitaji.

Binafsi, siamini kuwa kuna Muislamu anayeshindwa kutekeleza aina hizi za sadaka. Kama hivyo ndivyo, basi tujenge utamaduni wa kutoa sadaka kwa ikhlas na kwa nia ya kumridhisha Mwenyezi Mungu, bila kutarajia sifa au pongezi kutoka kwa watu.



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

ELIMU YA MAZISHI YA KIISLAMU

Mazishi kaburini: Kumweka maiti katika makazi yake ya mwisho

SEHEMU YA 11

Baada ya Swala ya Janaza na kuusindikiza mwili wa marehemu kwa heshima, hatua inayofuata ni kumweka kaburini. Hii ndiyo hatua ambayo mwanadamu humrudisha ndugu yake katika asili yake: udongo. Allah Mtukufu anasema: "Kutokana na udongo Tumekuumbeni, na humo Tutakurudisheni, na humo Tutakutoeni tena mara nyingine." [Qur'an, 20:55]. Aya hii inatukumbusha kwamba mwanadamu alianza safari yake kutoka katika udongo, na mwisho wa maisha yake hapa duniani ni kurudi humo. Lakini hata katika hatua hii ya mwisho, Uislamu haukuacha mambo bila mwongozo. Kuna adabu na taratibu zilizofundishwa ili kuhifadhi heshima ya marehemu.

Kaburi la Muislamu

Asili ni kwamba Muislamu azikwe katika makaburi ya Waislamu, pamoja na ndugu zake katika imani.

Makaburi katika Uislamu si mahali pa kufanya ibada kwa wafu, bali ni sehemu ya mapumziko ya miili yao na ukumbusho kwa walio hai.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Nilikuwa nimewakataza kutembelea makaburi, lakini sasa yazuruni kwani yanawakumbusha Akhera." [Muslim].

Kumuingiza maiti kaburini na dua yake

Anayemshusha maiti kaburini anapaswa kufanya hivyo kwa utulivu na heshima. Inapendekezwa kumlaza maiti kwa upande wake wa kulia, akielekea Qiblah.

Utaratibu huu umekuwa ukifuatwa na Waislamu wengi tangu zama za mwanzo, na wanazuoni pia wameutaja katika vitabu vyao vya fiqhi.

Wakati wa kumweka maiti kaburini, imepokewa kwamba Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Bismillahi wa 'ala millati Rasulillah" (yaani, Kwa jina la Allah na juu ya mila ya Mtume wa Allah). [Abu Daud na At-Tirmidhi].

Dua hii inatukumbusha kuwa hata hatua hii ya mwisho inafanywa kwa kumtegemea Allah.

Kufunika kaburi na kujaza udongo

Baada ya maiti kuwekwa kaburini, kaburi hufunikwa kwa udongo. Ni Sunnah kwa wanaohudhuria kushiriki katika kujaza udongo.

Imepokelewa kwamba Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alishiriki katika mazishi ya baadhi ya Maswahaba na alisimama karibu na kaburi.

Kitendo hiki kinaonyesha mshikamano wa Waislamu na unyenyekevu mbele ya mauti.

Kusimama baada ya kuzika na dua

Baada ya kumaliza mazishi, ni Sunnah kusimama karibu na kaburi na kumuombea marehemu.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alipomaliza kumzika mtu alisema: "Muombeeni ndugu yenu msamaha, na mumuombe athibitishwe kwani hivi sasa anaulizwa." [Abu Daud].

Hii inaonyesha kuwa wakati huo si wa kuondoka haraka, bali ni wa kumuombea marehemu.

Dua inayofaa baada ya mazishi ni kumuomba Allah amsamehe marehemu, amrehemu, amthibitishe katika kaburi na ampe mwisho mwema.

Ijulikane kuwa dua ndiyo zawadi kubwa ambayo walio hai wanaweza kumpelekea marehemu.

Suala la kusoma Qur'an kaburini

Wanazuoni wametofautiana kuhusu kusoma Qur'an karibu na kaburi baada ya mazishi.

Baadhi ya wanazuoni wameona kuwa inaruhusiwa au inapendekezwa katika mazingira fulani, huku wengine wakiona kuwa hakuna dalili sahihi ya kufanya hivyo kama ibada maalumu baada ya mazishi.

Kwa hiyo, jambo la msingi lililothibiti bila tofauti kubwa ni kumuombea marehemu, kumuombea msamaha na kufuata Sunnah zilizopokelewa.

Suala la Talqini baada ya kuzika

Baadhi ya Waislamu hufanya Talqini kwa marehemu baada ya kuzikwa, wakimkumbusha majibu ya maswali ya kaburini. Wanazuoni wametofautiana kuhusu suala hili.

Baadhi ya wanazuoni wa madhehebu fulani wameona kuwa kuna nafasi ya kufanya hivyo, wakitegemea baadhi ya athari na maana ya jumla ya nasaha. Wengine wameona kuwa hakuna dalili sahihi inayothibitisha kufanywa kwake na Mtume (Allah amshushie rehema na amani) au Maswahaba wake.

Kwa hiyo, ni suala la ikhtilafu ya kifiqhi, na halipaswi kuwa sababu ya kugombana au kuvunja umoja wa Waislamu.

Mambo yanayopaswa kuepukwa kaburini

Katika baadhi ya jamii, huonekana mambo yasiyo na msingi katika Sunnah, kama vile kupiga mayowe kaburini, kukaa kaburini kwa muda mrefu kwa kufuata desturi maalumu na kuweka chakula au vinywaji kwa ajili ya marehemu.

Mambo mengine yanayofanywa na baadhi ya watu lakini hayana msingi katika Sunnah ni kuwasha mishumaa, kuwaomba msaada waliokufa na kuyafanya makaburi kuwa mahali pa ibada.

Makaburi yanapaswa kubaki kuwa sehemu ya kumkumbuka Allah na kutafakari Akhera.

Funzo kutoka kaburini na hitimisho

Kaburi ni mahali ambapo tofauti zote za kidunia zinaisha. Hakuna tena cheo, mali, umaarufu wala nguvu. Kinachobaki ni imani na matendo.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alituambia tuyatembelee makaburi kwa sababu yanatukumbusha mwisho wetu.

Nihitimishe kwa kusema, mazishi ya Kiislamu yanaanza kwa huruma na kuishia kwa dua. Maiti anapoingizwa kaburini, wajibu wetu wa mwisho kwake si kupiga kelele wala kuomboleza kwa mayowe, bali ni kumuombea rehema kutoka kwa Mola wake.

Na Said Rajab

0783 650 803

SEHEMU YA 3

Miaka mitatu ya mateso Gaza, nini kifanyike?



Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulieleza kwamba licha ya uharibifu mkubwa uliotokea Gaza, ishara za amri na rehema za Mwenyezi Mungu zinaendelea kudhihirika. Tulibainisha kuwa watu wa Gaza, ambao wamepoteza karibu kila kitu, bado wanaendelea kuthibitisha kwa maneno na vitendo kwamba hawataiacha kamwe imani yao. Sasa tuendelee na sehemu inayofuata...

Suluhisho la Serikali mbili

Mpango wa kuanzisha mataifa mawili, Israel na Palestina, unaojulikana kwa Kiingereza kama 'Two–State Solution' hauleti ukombozi wa Palestina bali unazidisha na kuimarisha uvamizi na ukaliaji wa kimabavu wa ardhi ya Palestina unaofanywa na dola ya Kizayuni.

Mpango huu unahalalisha uwepo wa dola ya Kizayuni na kuhakikisha inaendelea kuwepo, huku ukiunda Mamlaka ya Palestina iliyo dhaifu, isiyo na uhuru wa kweli wala mamlaka kamili ya kujitawala.

Mpango huu wa hila unaimarisha hali iliyopo Palestina kwa kuipa sura mpya. Kwa kufanya hivyo, unayapa mataifa ya kibeberu fursa ya kujinasua kutokana na lawama za umwagaji damu wa Waislamu katika ardhi hii tukufu. Aidha, mpango huu unalenga kufanikisha jambo hatari zaidi: kuujengea umma wa Kiislamu utamaduni wa kukubali kushindwa na kukata tamaa katika mapambano ya kudai haki zake.

Hii ni kwa sababu kila kizazi kinapokubali maelewano yanayolegeza msimamo na kuridhia kuporwa kwa sehemu ya haki zake, maadui wa Uislamu hupata ujasiri wa kudai zaidi. Hatimaye, hali hiyo huwafanya Waislamu kupoteza mwelekeo na kuachana na njia wanayoiona kuwa ndiyo pekee ya kweli ya ukombozi.

Hili si jambo geni. Tangu mwaka 1959, Marekani imekuwa ikitekeleza kwa umakini mkubwa mkakati wa kuigeuza kadhia ya Wapalestina kuwa mradi unaodhibitiwa, kwa lengo la kuilinda dola ya Kizayuni katika Mashariki ya Kati, huku ikiutuliza umma wa Kiislamu kwa ahadi zisizotekelezeka za kuundwa kwa "dola" ya Palestina.

Kuanzia Mikataba ya Camp David hadi Makubaliano ya Oslo, na kutoka Makubaliano ya Abraham hadi mapendekezo ya Joe Biden na Donald Trump, kiini cha sera hii kimeendelea kuwa kilekile: Wapalestina huahidiwa mamlaka ya kujitawala bila kupewa uhuru kamili, huku wakiruhusiwa kuwa na jeshi la polisi lakini bila kuwa na jeshi la ulinzi.

Iwe ni Chama cha Republican kinachotawala Marekani kwa sasa au Chama cha Democratic kitakapoingia madarakani, sera ya taifa hilo kuhusu Palestina hubaki vilevile. Lengo kuu limeendelea kuwa kuimarisha ukaliaji wa mabavu wa Israel katika ardhi ya Palestina, kutuliza hasira za Waislamu na kuwafungia Wapalestina katika mazungumzo yasiyo na mwisho.

Kila Wapalestina wanapoinuka kudai haki zao, huibuka "suluhisho" jipya, iwe ni Mkataba wa Oslo, ramani ya njia (Roadmap), mazungumzo ya amani, makubaliano ya kusitisha mapigano au mpango wa Trump wa "Bodi ya Amani ya Gaza" wenye vipengele 20. Mipango hiyo huahidi maendeleo, lakini huishia kudumisha hali ileile ya kudumaa bila kuleta mabadiliko ya msingi.

Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah

TAFAKURI YA WIKI
NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

Laiti ningekuwa kama hawa!

Kuna watu ninapowaona, moyo wangu hujaa wivu. Si wivu wa kutamani wapoteze walichonacho, bali wivu wa kutamani Mwenyezi Mungu anijaalie kile alichowajaalia. Wivu unaonifanya nijitazame, nijitathmini na wakati mwingine nijisikie maskini katikati ya riziki si haba aliyonipa Allah Mtukufu. Siwaonei wivu matajiri, viongozi, wasomi au watu maarufu. Ninaowaonea wivu, wengi, ni vijana wadogo ambao pengine hawana pesa lakini wana utajiri ambao fedha haziwezi kuununua.

Waliohifadhi Qur'an yote

Mosi, ninawaonea wivu walioihifadhi Qur'an yote vifuani mwao. Ninapokutana na kijana anayesoma aya kutoka sura yoyote bila kufungua Msahafu, moyo wangu hujawa furaha.

Fikiria! Maneno ya Allah, kuanzia Al-Fatiha hadi An-Nas, yamepata makazi ndani ya moyo wa mwanadamu. Mimi hata juzuu moja sijaweza kuihifadhi! Laiti ningekuwa mmoja wao! Laiti ulimi wangu ungekuwa rafiki wa Qur'an, na kifua changu maktaba ya maneno ya Allah!

Wanaosali alfajr kwa wakati

Nawaonea wivu wanaoswali Alfajiri kwa wakati, hasa msikitini. Si kwamba swala nyingine hazina umuhimu. La hasha! Lakini Alfajiri ina mtihani wake wa pekee.

Ni rahisi kuzungumza kuhusu mapenzi ya Allah ukiwa macho. Mtihani huja pale usingizi unapokuwa mtamu, godoro lina joto, mwili umechoka na macho yanakataa kufunguka.

Pengine umelala saa nane usiku. Pengine umechoshwa na shughuli za jana. Lakini adhana inapolia, unaamka na kuacha kitanda chako kwa ajili ya Mola wako. Ninawaonea wivu watu hao! Wamejifunza kuutii mwito wa Allah hata pale nafsi inapowashawishi kuendelea kulala.

Wajuzi wa lugha ya Kiarabu

Tatu, ninawaonea wivu wanaoielewa lugha ya Kiarabu, lugha ya Qur'an.

Ninapomsikia imamu akisoma Qur'an, mimi wakati mwingine nasubiri tafsiri ili kuelewa ujumbe. Lakini pembeni yangu yupo kijana anayeelewa kila neno, kila onyo na kila bishara.

Anaposikia aya inayozungumzia Pepo, anaelewa. Inapotajwa adhabu, anaelewa. Anaposikia dua ya Nabii, moyo wake unaguswa moja kwa moja na maana yake.

Laiti ningekuwa na ufunguo huo wa kuifungua hazina ya Qur'an!

Wanaofanya toba ya kweli

Nne, ninawaonea wivu waliotubia kwa dhati na kuachana na madhambi yao. Sizungumzii watu wasiokosea. Hakuna mwanadamu aliyekingwa na makosa. Ninazungumzia wale walioanguka, wakatambua makosa yao, wakamrudia Allah kwa machozi ya kweli na kuazimia kutorudia dhambi hiyo.

Watu walioweza kuvunja minyororo ya mazoea mabaya. Walioachana na starehe ya haramu hata kama mioyo yao ilikuwa imeizoea.

Mimi najua jinsi nafsi inavyoweza kumshawishi mwanadamu kurudia kosa alilokwisha kulijutia. Ndiyo maana ninawaheshimu waliofanikiwa kuishinda nafsi katika mapambano hayo.

Walioshikamana na funga

Tano, ninawaonea wivu wanaofunga Jumatatu, Alhamisi na siku nyeupe za kila mwezi wa Kiislamu na masiku mengine matukufu yaliyotajwa katika Qur'an na Sunna.

Watu hawa wanaishi katika dunia ambayo chakula kinapatikana, lakini wanachagua kukiacha kwa ajili ya Allah.

Wanakabiliwa na kiu, njaa, kazi na majukumu ya kila siku, lakini hawatafuti visingizio. Wameifanya saumu ya Sunna kuwa sehemu ya maisha yao.

Wengine wanapanga ratiba zao kwa kuangalia tarehe za mishahara. Wao wanakumbuka pia tarehe 13, 14 na 15 za mwezi wa Kiislamu. Huo ni utajiri wa ajabu!

Waamkao kwa Tahajjud

Sita, katika ninawaonea wivu ni wale wanaodumu katika Tahajjud. Dunia inapolala, wao wanaamka. Wakati wengine wanapumzika, wao wanasimama mbele ya Mola wao.

Hakuna kamera, hakuna makofi wala sifa za watu. Ni mja na Muumba wake, katika utulivu wa usiku. Wanamsimulia Allah huzuni zao, wanamuomba msamaha na wanamshukuru kwa neema zake.

Ninapotafakari ibada hiyo, najiuliza: Mimi ninapataje nguvu za kukesha kwa mambo ya dunia, lakini ninashindwa kutenga hata dakika chache za usiku kwa ajili ya Allah?

Wanaochunga mipaka ya sharia

Saba, ninawaonea wivu wanaochunga mipaka ya halali na haramu katika kila jambo. Hawa hawajiulizi tu, "Nitapata faida kiasi gani?" Wanajiuliza kwanza, "Je, Allah ameruhusu?"

Wanachunguza wanachokula, wanachovaa, wanachouza, wanachonunua na namna wanavyopata fedha. Wanaogopa riba, rushwa, udanganyifu na kipato kisicho halali.

Hata wanapokuwa peke yao, wanajitahidi kumcha Allah. Hawapimi uhalali wa jambo kwa idadi ya watu wanaolifanya.

Utajiri katika wema

Na mwisho, ninapowatazama watu hawa, ninajifunza jambo moja: si kila mtu ninayepaswa kumuonea wivu ana gari zuri, nyumba kubwa au akaunti yenye mamilioni.

Wengine wana utajiri uliojificha katika nyoyo zao. Sitaki neema zao zipungue. Natamani ziongezeke, na mimi nipewe sehemu ya kheri hiyo.

Na ninapotambua kuwa bado sijafikia walipofikia, najikumbusha kwamba mlango wa kujirekebisha haujafungwa.

Naweza kuanza leo. Kwa aya moja. Kwa Alfajiri moja. Kwa saumu moja. Kwa toba ya kweli. Kwa rakaa mbili za usiku. Kwa kukataa kipato cha haramu.

Huenda nisiwe kama wao kesho, lakini sitaki kuwa yuleyule wa jana.

Ewe Allah, waongezee kheri wale ninaowaonea wivu kwa ajili Yako. Na mimi usiniache kuwa mtazamaji wa wema wao maisha yangu yote. Nijaalie niwe mmoja wao. Amin.

Na Samrath Msuya

0789 201 383

Msaidie mtoto mpweke kupata marafiki kujiamini



“Mama, leo hakuna mtoto aliyetaka kucheza na mimi.” Maneno haya yanaweza kumuumiza mzazi anayetamani kumwona mwanawe akiwa na furaha, akipendwa na kukubalika na wenzake.

Hata hivyo, kupata marafiki si jambo rahisi kwa kila mtoto. Wengine huanzisha urafiki haraka, huku wengine wakihitaji muda mrefu kabla ya kujisikia huru mbele ya wenzao.

Urafiki ni sehemu muhimu ya ukuaji wa mtoto. Kupitia mahusiano na watoto wengine, anajifunza kuwasiliana, kushirikiana, kutatua migogoro, kuheshimu tofauti na kuelewa hisia za wengine.

Umuhimu wa urafiki huongezeka hasa katika umri wa miaka mitano hadi 12, watoto wanapoanza kujenga mahusiano yanayozidi michezo ya kawaida. Wataalamu wa malezi wanasisitiza kwamba uwezo wa kujenga urafiki unaweza kuimarishwa kupitia mazoezi, mifano mizuri na mazingira yanayompa mtoto nafasi ya kushirikiana na wengine.

Kwa nini baadhi ya watoto hushindwa kupata marafiki?

Kuna sababu mbalimbali zinazoweza kumfanya mtoto apate ugumu wa kuanzisha au kudumisha urafiki. Baadhi ni aibu, wasiwasi wa kukataliwa, matatizo ya mawasiliano na kushindwa kuelewa hisia au ishara za wengine.

Watoto wengine hushindwa kudhibiti hasira au kukatishwa tamaa, jambo linaloweza kusababisha migogoro wanapocheza na wenzao.

Wengine hukosa fursa za kutosha za kukutana na watoto wa umri wao, hivyo wanakuwa na uzoefu mdogo wa kushirikiana katika michezo na mazungumzo.

Hata hivyo, kuwa na marafiki wachache si lazima kuashirie tatizo. Baadhi ya watoto hufurahia kuwa na rafiki mmoja au wawili wa karibu kuliko kushiriki katika makundi makubwa.

Namna wazazi wanavyoweza kuwasaidia watoto

Mosi, usichanganye aibu na kushindwa kupata marafiki. Si kila mtoto anayependa kukaa kimya ana tatizo la kijamii.

Mzazi hapaswi kumlazimisha mtoto kuwa mchangamfu kama wenzake. Badala yake, amsaidie kujenga mahusiano yanayomfanya ajisikie salama na mwenye furaha.

Pili, mfundishe namna ya kuanzisha mazungumzo. Kwa watu wazima, kumsalimia mtu au kuanzisha mazungumzo kunaweza kuonekana jambo rahisi. Kwa mtoto mwenye aibu, hatua hiyo inaweza kuwa changamoto kubwa.

Mzazi anaweza kumfundisha kutumia kauli kama, “Naweza kucheza nanyi?” au “Ungependa tucheze pamoja?” Mazoezi yanaweza kufanyika nyumbani kupitia mchezo wa kuigiza, ambapo mzazi na mtoto wanabadilishana nafasi za kuanzisha mazungumzo.

Tatu, mpe fursa za kukutana na watoto wengine. Urafiki haujengwi shuleni pekee.

Michezo ya pamoja, shughuli za michezo, sanaa, madrasa na mikusanyiko ya kifamilia vinaweza kuwapa watoto nafasi ya kuzoeana. Kwa mtoto anayesita kujiunga na kundi kubwa, mzazi anaweza kuanza kwa kumwalika mtoto mmoja nyumbani kwa mchezo unaosimamiwa.

Nne, kuwa mfano wa mahusiano mazuri. Watoto hujifunza namna ya kuwatendea wengine kwa kutazama watu wazima.

Mzazi anayesalimia majirani, kusikiliza wengine, kuomba msamaha na kutatua tofauti kwa utulivu anamfundisha mtoto stadi muhimu za kijamii. Hata mazungumzo ya kawaida nyumbani yanaweza kumfundisha mtoto kusubiri zamu yake ya kuzungumza na kuheshimu maoni tofauti.

Tano, mfundishe kutatua migogoro. Kutofautiana, kugombania vifaa vya kuchezea au kukataliwa kushiriki mchezo ni sehemu ya uzoefu wa watoto.

Badala ya mzazi kuingilia kila ugomvi, anaweza kumuuliza mtoto kilichotokea, jinsi mwenzake alivyojisikia na hatua inayoweza kurejesha maelewano. Mtoto anapaswa kujifunza kuomba msamaha, kusikiliza na kukubaliana. Hata hivyo, unyanyasaji au vitisho vinahitaji hatua za watu wazima.

Sita, mjengee kujiamini hatua kwa hatua. Mtoto mwenye wasiwasi wa kushirikiana na wengine anaweza kuanza kwa kusalimia jirani, kisha kuzungumza na mtoto mmoja kabla ya

NA ZAHARANI BARAKA

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

Dunia ni dhalili kuliko mbuzi huyu

Kutoka kwa Jabir bin Abdillah (Allah amridhie) amesimulia kuwa Mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie) alipita sokoni akitokea Al–'Aliyah, huku watu wakiwa wamemzunguka.

Akiwa njiani, aliona mbuzi aliyekufa (mzoga) mwenye masikio madogo au yaliyokatika, akamshika sikio kisha akasema: "Ni nani kati yenu angependa kumiliki mbuzi huyu kwa dirham moja?" Wakasema: "Hatupendi kuwa naye kwa chochote, tutamfanyia nini?"

Mtume akauliza: "Je, mngependa awe wenu (niwape bure)?" Wakamjibu: "Wallahi, hata kama angekuwa hai, bado angekuwa na kasoro kwa sababu ya udogo wa masikio yake. Itakuwaje sasa akiwa amekufa?"

Mtume (rehema na amani zimshukie) akasema: "Wallahi, dunia hii haina thamani mbele ya Allah kuliko mbuzi huyu alivyo duni kwenu."[Muslim].

Mafundisho ya tukio hili

Muislamu hapaswi kuifanya dunia kuwa lengo kuu la maisha yake, bali anapaswa kuitumia kama njia ya kumtii Allah na kujiandaa kwa maisha ya Akhera. Ni muhimu kusoma, kufanya kazi na kutafuta riziki ya halali, lakini shughuli hizo hazipaswi kumfanya apuuze ibada, wajibu wa kidini na matendo mema.

Haifai kujishughulisha kupita kiasi na kutafuta mali hadi kusahau ibada, familia na wajibu mwingine muhimu.

Ishi kama mgeni

Ibn Umar (Allah amridhie) amesema siku moja Mtume (rehema na amani zimshukie) alimshika bega na kumwambia: "Ishi duniani kama mgeni au mpita njia. Inapoingia jioni usitarajie kufika asubuhi, na unapoamka asubuhi usitarajie kufika jioni. Tumia afya yako kabla ya kuugua, na maisha yako kabla ya kufa. [Bukhari].

Katika hadith nyingine, Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Mwenye kuifanya dunia kuwa ndiyo hamu yake kuu, Allah atayatawanya mambo yake, ataweka umasikini mbele ya macho yake, na hatopata katika dunia isipokuwa kile alichoandikiwa. Na mwenye kuifanya Akhera kuwa ndiyo hamu yake kuu, Allah atamkusanyia mambo yake, ataweka utajiri moyoni mwake, na dunia itamjia ikiwa imenyenyekea kwake." [Ibn Majah].

Kupitia hadith hizi mbili, Mtume anaonya kuwa kuifanya dunia kuwa lengo kuu la maisha kunaweza kumwingiza mtu katika tamaa zisizo na mwisho na kumfanya asahau maandalizi ya maisha ya Akhera.

Muislamu anapaswa kufanya kazi kwa bidii na kutafuta riziki ya halali bila kusahau Akhera. Pia, anatakiwa kutumia muda wake kufanya matendo mema badala ya kuahirisha ibada na toba kwa kutegemea kuwa bado ana muda mwingi wa kuishi.

Kuridhika kama kinga dhidi ya tamaa za dunia

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Lau mwanadamu angekuwa na mabonde mawili ya dhahabu, bado angetamani kuwa na la tatu. Hakuna kinachojaza tumbo la mwanadamu isipokuwa udongo, na Allah humsamehe mwenye kutubia." [Muslim].

Hadith hii inatufundisha kuwa mali nyingi haziwezi kumaliza tamaa ya mwanadamu ikiwa hajajifunza kuridhika na kile alichonacho. Aidha, Mtume ameeleza kuwa mwanadamu anapozeeka, bado huendelea kuwa na pupa ya kutafuta mali na matumaini ya kuishi muda mrefu. [Bukhari].

Kwa msingi huo, ni muhimu kutafuta riziki kwa njia halali, kutumia mali katika mambo ya kheri na kujiepusha na tamaa zinazoweza kututawala. Vilevile, hatupaswi kuahirisha toba, ibada na matendo mema kwa kutegemea kuwa tutaishi muda mrefu.

Linganisha neema zako na walio chini yako

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Waangalieni walio chini yenu, wala msiwaangalie walio juu yenu, kwa sababu kufanya hivyo kunafaa zaidi ili msizidharau neema za Allah alizowapa." [Muslim].

Katika suala la mali na maisha, tunapaswa kuwatazama watu walio katika hali ngumu zaidi kuliko sisi ili tujifunze kuthamini na kushukuru kwa neema tulizojaliwa na Allah. Kujilinganisha kila mara na wenye mali nyingi kunaweza kuongeza tamaa na kutufanya tusithamini tulichonacho.

Hata hivyo, kuridhika hakumaanishi kukubali hali ngumu bila kufanya juhudi za kuiboresha. Muislamu anapaswa kujitahidi kuinua hali yake ya maisha kwa njia halali, bila kudhulumu, kudanganya au kuvuka mipaka ya Allah.

Katika kutafuta radhi za Allah na kufanya matendo mema, tunapaswa kujifunza kutoka kwa wale waliotutangulia katika kheri na kujitahidi kuiga mifano yao bora.

Tujihadhari na fitina ya mali

Tuondoe shaka ya umasikini na ufukara, kwani Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Furahini na tarajieni mema. Ufukara si kitu ninachokihofia kwenu, bali ninachohofia ni dunia kufunguliwa na kuletwa kwenu kwa wingi, kisha mkashindana kuipata kama walivyoshindana watu waliowatangulia, na hatimaye ikawaangamiza kama ilivyowaangamiza wao." [Bukhari na Muslim].

Ujumbe huu unatukumbusha kuwa mali ni neema inayohitaji hekima na uwajibikaji. Tunapaswa kuitafuta kwa njia halali, kuitumia katika mambo yenye manufaa na kuwasaidia wenye mahitaji.

Zaidi ya yote, tusiruhusu mashindano ya kutafuta mali yatutenganishe na Allah, yatufanye tusahau wajibu wetu au yatuchochee kufanya mambo yanayopingana na maadili ya Kiislamu. Ni muhimu kutambua kuwa mafanikio ya kweli hayapimwi kwa wingi wa mali pekee, bali ni kuwa na moyo wa kuridhika, kutafuta riziki ya halali, kutekeleza wajibu na kujiandaa kwa maisha ya Akhera.

Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

Siri ya viongozi wanaopendwa na kuaminiwa

Kwa nini baadhi ya viongozi hupendwa na kuaminiwa, huku wengine wakiogopwa na wafanyakazi wao? Kuna viongozi ambao wafanyakazi wao hujituma hata wasiposimamiwa, huwatetea wanapokosolewa na kushirikiana nao wakati wa matatizo. Lakini wapo wengine ambao wafanyakazi huwatii kwa kuogopa kufukuzwa, kuadhibiwa au kunyimwa fursa. Wakiondoka ofisini, kila mtu anapumua!

Ukweli ni kwamba cheo kinaweza kumpa mtu mamlaka, lakini hakiwezi kumhakikishia kupendwa na kuaminiwa.Mwandishi Harvey Deutschendorf, katika makala yake 7 Habits of Leaders Who Inspire Loyalty, iliyochapishwa na Fast Company mwaka 2015, anaeleza tabia zinazojenga uaminifu wa wafanyakazi.

Naye mtaalamu wa uongozi Carol Kinsey Goman, akiandika katika Forbes mwaka huohuo, anasisitiza umuhimu wa mahusiano, kuheshimiana na kujali wengine.

Mitazamo hiyo inaonyesha mambo kadhaa yanayowatofautisha viongozi wanaoaminiwa na wanaoogopwa.

Mosi, wanatenda wanayoyasema. Hakuna kinachoharibu uaminifu kama kiongozi anayehubiri uadilifu huku akipendelea watu wake, au anayehimiza uwajibikaji lakini hakubali makosa yake.

Viongozi wanaoaminiwa hutimiza ahadi, hukiri makosa na kutumia viwango vinavyofanana kwao na kwa wengine.

Pili, wanawaamini wafanyakazi wao. Baadhi ya viongozi hudhani kusimamia kila jambo dogo kunahakikisha kazi zinafanyika vizuri.

Lakini usimamizi wa kupita kiasi huwafanya wafanyakazi wajione hawana uwezo wa kufanya maamuzi.

Kiongozi anayejenga uaminifu huwapa watu majukumu na nafasi ya kuonyesha uwezo wao. Wanapokosea, huwasaidia kujirekebisha badala ya kuwafedhehesha.

Tatu, wanajali maendeleo ya wengine. Viongozi bora hawawaoni wafanyakazi kama vifaa vya kutimiza malengo yao.

Huwasaidia kujifunza, kupata uzoefu na kujiandaa kwa majukumu makubwa. Deutschendorf anasisitiza kwamba kiongozi hapaswi kuogopa mfanyakazi wake kuwa bora zaidi au kupata fursa nyingine.

Nne, wanasikiliza na kushirikisha. Kiongozi anayefanya maamuzi yote peke yake anaweza kupata utiifu, lakini si lazima ajenge moyo wa kujitolea.

Wafanyakazi wanaposhirikishwa, huona mafanikio ya taasisi kama yao pia. Kusikiliza hakumaanishi kukubali kila pendekezo, bali kuthamini mawazo na kueleza sababu za maamuzi.

Tano, wanawajua wafanyakazi kama binadamu. Mfanyakazi si jina kwenye orodha ya mishahara pekee. Ana familia, matarajio na changamoto binafsi.

Goman anasimulia kuhusu meneja aliyewafahamu wafanyakazi wake 125, si kwa majukumu yao tu, bali pia mambo muhimu yaliyokuwa yakiendelea katika maisha yao.

Kuwajali hakumaanishi kuingilia faragha zao, bali kuwaheshimu na kuwasaidia inapowezekana.

Sita, wanakuwa sehemu ya timu. Viongozi wanaoheshimika hawajioni kuwa juu ya kila kazi. Wakati wa matatizo, hushirikiana na wafanyakazi kutafuta ufumbuzi badala ya kutoa maagizo kutoka mbali.

Hivyo huonyesha kuwa wanathamini mchango wa wengine na wako tayari kubeba sehemu ya mzigo.

Saba, wanajenga mazingira salama ya kusema ukweli. Wafanyakazi wanaoogopa kuadhibiwa wanapokiri makosa au kutoa maoni wanaweza kuchagua kunyamaza.

Ukimya huo huficha matatizo ambayo yangeweza kutatuliwa mapema.

Viongozi wanaoaminiwa hukubali kukosolewa, husikiliza taarifa zisizowafurahisha na kutofautisha makosa ya kujifunza na uzembe unaohitaji uwajibikaji.

Nane, wanatoa mwelekeo na kutia moyo. Wafanyakazi wanahitaji kujua wanachokifanya, umuhimu wake na namna kinavyochangia malengo ya taasisi.

Kiongozi mwenye maono yanayoeleweka, anayethamini mafanikio na kutia moyo, anaweza kuchochea juhudi ambazo haziwezi kupatikana kwa vitisho pekee.

Uaminifu hauwezi kulazimishwa

Hata hivyo, uaminifu si kukubali kila jambo bila kuuliza maswali. Mfanyakazi anaweza kuwa mwaminifu huku akipinga uamuzi usiofaa.

Vilevile, kiongozi mwenye mahusiano mazuri bado anahitaji uwezo wa kitaaluma, haki na uwajibikaji. Ukarimu hauwezi kufidia maamuzi mabovu.

Hatimaye, tofauti kati ya viongozi wanaopendwa na wanaoogopwa ni namna wanavyotumia mamlaka yao.

Wengine hutumia vitisho kuwalazimisha watu kuwafuata; wengine hujenga mazingira yanayowafanya watu watake kushirikiana nao.

Cheo kinaweza kukupa mamlaka ya kuamrisha watu, lakini hakiwezi kukupa nafasi katika mioyo yao. Nafasi hiyo hujengwa kwa matendo, si amri.



MAKALA

MALEZI

NA JUNAYNAT ALLY DAMA

0789 201 383

Malezi katika mbio za kusaka na ubize mwingi

Kwa mtazamo wa Kiislamu, watoto ni amana kutoka kwa Allah. Qur'an inasema: "Enyi mlioamini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto" [Qur'an, 66:6]. Wajibu huu hauishii katika kuwapatia watoto chakula, mavazi na elimu, bali unahusisha kujenga imani, tabia na mwenendo wao.

Hakuna ubaya kwa mzazi kufanya kazi kwa bidii ili familia yake ipate maisha bora. Tatizo huanza pale ambapo kutafuta fedha kunachukua nafasi kubwa kiasi cha kumwacha mtoto bila muda, mwongozo na ukaribu wa wazazi wake. Katika mazingira hayo, changamoto mbalimbali za malezi hujitokeza.

Mosi, kutanguliza mali kuliko malezi. Katika jamii inayopima mafanikio kwa utajiri na anasa, baadhi ya wazazi huamini kwamba kumpatia mtoto kila anachotaka ndiyo malezi bora.

Wanaweza kutumia muda mwingi kutafuta fedha za kumnunulia simu ya gharama kubwa, mavazi ya kifahari na vitu vingine, huku wakikosa muda wa kumfundisha kuridhika, kushukuru na kuwajali wengine.

Kupitia matangazo na mitandao ya kijamii, watoto nao huvutiwa na maisha ya anasa. Bila mwongozo wa wazazi, wanaweza kukua wakiamini kuwa thamani ya mwanadamu hupimwa kwa mali alizonazo.

Pili, kukabidhi malezi kwa wafanyakazi wa nyumbani. Katika harakati za kutafuta riziki, baba na mama wanaweza kuondoka nyumbani asubuhi na kurejea usiku.

Watoto hubaki na wafanyakazi wa nyumbani wanaowasaidia kula, kuoga, kuvaa na kutekeleza shughuli nyingine za kila siku.

Msaada huo ni muhimu, lakini changamoto hujitokeza pale mfanyakazi anapogeuka kuwa mlezi mkuu, huku wazazi wakibaki kuwa watoaji wa fedha.

Tatu, teknolojia kuchukua nafasi ya wazazi. Wazazi wanapokuwa na shughuli nyingi, simu na televisheni zinaweza kutumiwa kuwafanya watoto watulie na kujiburudisha.

Ingawa teknolojia ina manufaa ya kielimu, matumizi yasiyo na mwongozo yanaweza kuwafundisha watoto mitazamo inayopingana na maadili ya familia.

Badala ya kutumia vifaa hivyo kama mbadala wa malezi, wazazi wanapaswa kufuatilia maudhui, kuweka mipaka na kuzungumza na watoto kuhusu wanachojifunza.

Nne, kuwekeza katika ufaulu kuliko tabia. Katika jitihada za kuwajengea watoto maisha bora ya baadaye, wazazi huwekeza fedha nyingi katika shule nzuri, masomo ya ziada na maandalizi ya mitihani.

Hata hivyo, kulipa ada kubwa hakumhakikishii mtoto kupata malezi bora. Anaweza kufaulu darasani lakini akakosa nidhamu, heshima na uwezo wa kujitegemea.

Elimu bora inahitaji ushiriki wa wazazi katika kujenga maarifa, maadili na uwajibikaji.

Tano, kuwaacha watoto chini ya ushawishi wa marafiki. Wazazi wanapokosa muda wa kuzungumza na watoto, nafasi hiyo inaweza kuchukuliwa na marafiki.

Watoto wanapokua, hutamani kukubalika katika makundi yao. Wanaweza kuiga matumizi ya fedha, mavazi na tabia zisizolingana na misingi ya familia.

Badala ya kutegemea makatazo pekee, wazazi wanahitaji kujenga ukaribu unaowawezesha watoto kuwashirikisha changamoto zao na kupata mwongozo wa kufanya maamuzi sahihi.

Sita, kupungua kwa mawasiliano ya kifamilia. Pilikapilika za kazi zinaweza kuifanya familia kuishi nyumba moja bila kuwa na muda wa kutosha wa kuzungumza.

Baba anakuwa na shughuli zake, mama anashughulika na majukumu mengine, huku watoto wakijikita kwenye simu au televisheni.

Mawasiliano yanapopungua, wazazi wanaweza kuchelewa kutambua hofu, matatizo ya shuleni na changamoto nyingine zinazowakabili watoto.

Saba, kushindwa kuwa mfano mwema. Katika mbio za kutafuta mafanikio, wazazi wanapaswa kukumbuka kuwa watoto hujifunza zaidi kutokana na matendo kuliko maelekezo.

Mzazi anayemfundisha mtoto uaminifu lakini anatumia udanganyifu kupata fedha anampa ujumbe unaokinzana. Vivyo hivyo, mzazi anayemkataza mtoto kutumia simu kupita kiasi huku yeye mwenyewe akiitumia muda wote.

Qur'an, katika Surat Luqman [31:13–19], inaonyesha umuhimu wa kumjengea mtoto imani, ibada, subira, unyenyekevu na adabu.

Nane, kutumia fedha kumrahisishia mtoto kila jambo. Baadhi ya wazazi, kwa sababu ya shughuli nyingi au kutaka watoto wao wasipitie shida walizopitia wao, huwapatia kila kitu na kuwaondolea majukumu yote.

Mtoto anaweza kukua akiwa na mahitaji yote, lakini hajui kutunza vitu vyake, kufanya usafi au kusaidia kazi ndogo za nyumbani. Malezi bora yanahitaji kumpa mtoto majukumu yanayolingana na umri wake ili ajifunze kujitegemea na kuwajibika.

Nihitimishe kwa kusisitiza kuwa kutafuta mali na kuwapatia watoto maisha bora ni wajibu muhimu wa wazazi, lakini juhudi hizo hazipaswi kuwafanya wasahau jukumu lao la msingi la malezi.

Fedha zinaweza kununua chakula, mavazi, nyumba na elimu nzuri, lakini haziwezi kuchukua nafasi ya upendo, muda, mazungumzo na mfano mwema wa mzazi.

Na Samrath Msuya
0789 201 383

Ma 'genius' huzaliwa hivyo au hutengenezwa?

Albert Einstein, Isaac Newton, Leonardo da Vinci na Marie Curie ni miongoni mwa watu wanaotajwa sana katika historia kutokana na uwezo wao wa kipekee wa kufikiri, kubuni na kufanya ugunduzi uliobadilisha dunia. Lakini swali moja limeendelea kuwavutia wanasayansi, wanasaikolojia na wataalamu wa elimu: Je, watu hawa walizaliwa na akili za kipekee, au walifikia kiwango hicho kutokana na elimu, mazingira na juhudi zao? Swali hili linahusiana na mjadala wa muda mrefu katika saikolojia unaojulikana kama nature versus nurture, yaani mchango wa urithi wa kinasaba dhidi ya mazingira katika kumjenga binadamu.

Utafiti wa kisasa unaonyesha kwamba uwezo wa kiakili hutokana na mwingiliano wa vinasaba, mazingira, mazoezi na fursa. Hata hivyo, mchango wa kila kipengele hutofautiana kati ya watu na aina za uwezo.

Je, akili za kipekee hurithiwa?

Tafiti zinazohusisha mapacha na watoto waliolelewa na wazazi wasio wa kuwazaa zinaonyesha kwamba vinasaba vina mchango mkubwa katika tofauti za uwezo wa kiakili.

Baadhi ya makadirio yanaonyesha kwamba karibu asilimia 50 ya tofauti za alama za vipimo vya akili, vinavyojulikana kama IQ, katika makundi fulani ya watu zinaweza kuhusishwa na tofauti za kinasaba.

Hii haimaanishi kwamba asilimia 50 ya akili ya mtu mmoja imetokana na vinasaba. Wala haimaanishi kwamba uwezo wake hauwezi kubadilika.

Kwa mfano, baadhi ya watoto huonyesha uwezo mkubwa wa kuelewa hesabu, lugha au muziki wakiwa wadogo, kabla hawajapata mafunzo ya kina.

Hata hivyo, kuwa na uwezo mkubwa wa kuzaliwa hakuhakikishi mafanikio makubwa baadaye. Kipaji kinaweza kudumaa ikiwa hakitapata mazingira yanayokiendeleza.

Nafasi ya mazoezi na juhudi

Mwanasaikolojia K. Anders Ericsson alifanya tafiti kuhusu namna watu wanavyofikia viwango vya juu vya utaalamu katika muziki, michezo na taaluma nyingine.

Alisisitiza umuhimu wa deliberate practice, yaani mazoezi yenye malengo maalumu, mrejesho na jitihada za kurekebisha udhaifu.

Dhana maarufu ya saa 10,000, iliyoenezwa na mwandishi Malcolm Gladwell, ilitokana kwa kiasi fulani na tafiti hizo.

Hata hivyo, Ericsson hakuthibitisha kwamba kila mtu akifanya mazoezi kwa saa 10,000 lazima awe gwiji. Utafiti unaonyesha kwamba mazoezi ni muhimu, lakini hayatoshi kueleza tofauti zote za mafanikio.

Mfano ni Wolfgang Amadeus Mozart, aliyeonyesha kipaji cha muziki akiwa mtoto, lakini pia alipata mafunzo makubwa kutoka kwa baba yake na kufanya mazoezi kwa miaka mingi.

Kwa hiyo, kipaji kinaweza kumpa mtu mwanzo mzuri, lakini juhudi na mafunzo humsaidia kukiendeleza.

Mazingira yanaweza kubadilisha akili?

Ushahidi mwingine unatokana na jambo linaloitwa Flynn Effect, lililopewa jina la mtafiti James Flynn. Katika nchi nyingi, alama za IQ ziliongezeka kwa miongo kadhaa, wakati mwingine kwa wastani wa takribani pointi tatu kila muongo.

Mabadiliko hayo yalitokea kwa kasi isiyoweza kuelezwa kwa mabadiliko ya vinasaba pekee.

Watafiti wamehusisha ongezeko hilo na mambo kama elimu, lishe bora, afya na mazingira yanayohitaji matumizi makubwa ya fikra.

Hata hivyo, ongezeko hilo halijaendelea katika nchi zote. Baadhi zimeonyesha kudorora kwa alama katika miaka ya karibuni.

Jambo muhimu ni kwamba mazingira yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa uwezo unaopimwa na vipimo vya akili.

Je, mtu mwenye akili za kipekee ana sifa gani?

Wataalamu hutaja baadhi ya tabia zinazoweza kusaidia kukuza uwezo wa kipekee.

Mosi, udadisi. Watu wabunifu huwa na hamu kubwa ya kuuliza maswali, kuchunguza mambo na kutafuta majibu ambayo wengine hawajayafikiria.

Pili, uvumilivu. Mafanikio makubwa mara nyingi hutanguliwa na makosa, kushindwa na majaribio mengi.

Tatu, ubunifu. Uwezo wa kuona tatizo kwa mtazamo tofauti na kuunganisha mawazo yasiyohusiana moja kwa moja unaweza kuzalisha ugunduzi.

Nne, kujifunza bila kuchoka. Kusoma, kufanya majaribio na kupokea ukosoaji husaidia kupanua maarifa na kurekebisha fikra.

Tano, mazingira yenye msaada. Walimu wazuri, wazazi wanaotia moyo, washauri na taasisi zinazothamini ubunifu vinaweza kusaidia vipaji kustawi.

Hatari ya kuabudu watu wenye akili za kipekee

Katika kitabu The Genius Myth, mwandishi Helen Lewis anahoji tabia ya jamii kuwachukulia watu wenye mafanikio makubwa kama viumbe wenye uwezo wa kipekee katika kila jambo.

Anasisitiza kwamba nyuma ya mafanikio yao mara nyingi kuna walimu, familia, wafanyakazi wenzao na taasisi ambazo mchango wake husahaulika.

Aidha, alama kubwa za IQ hazimaanishi kwamba mtu ana hekima, maadili bora au uwezo wa kufanya maamuzi sahihi katika kila eneo. Kwa hiyo, shule zinapaswa kutambua vipaji bila kuwafanya watoto wengine wajione hawana uwezo.

Hatimaye, swali si kama mtu mwenye akili za kipekee huzaliwa au hutengenezwa. Ushahidi unaonyesha kwamba vipaji vya kuzaliwa na mazingira hushirikiana. Jamii inayowekeza katika elimu, lishe, ubunifu na fursa inaweza kusaidia uwezo mwingi uliojificha kujitokeza.

VISION 2050

جُمادى الأول

TUJIFUNZE

AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

Uandishi wa habari kwa msaada wa AI

SEHEMU YA

9

Usimpe AI siri zako: Linda vyanzo, faragha na taarifa nyeti

Mwandishi anaweza kuitumia akili bandia (AI) kurekebisha maandishi, kufupisha nyaraka, kunukuu mahojiano au kupanga taarifa. Lakini urahisi huo unaibua swali muhimu: Ni taarifa gani hatupaswi kuziingiza kwenye AI?

Katika uandishi wa habari, swali hili ni nyeti. Waandishi hushughulikia majina, namba za simu, nyaraka za siri, madai yanayochunguzwa na watu ambao usalama wao unategemea kutotambulika.

Kabla ya kutumia AI, jiulize: Nikishindwa kudhibiti taarifa hii baada ya kuiingiza, madhara yatakuwa nini?

Si kila taarifa ni hatari kuiweka kwenye AI. Taarifa za jumla, mawazo ya makala, maswali ya kielimu na maandishi yasiyo ya siri yanaweza kushirikishwa kwa tahadhari.

Hata hivyo, taarifa binafsi kama majina, anuani, namba za simu na maelezo ya kifamilia zinahitaji uangalifu, hasa zinapoweza kumtambulisha mtu.

Taarifa nyeti zaidi, zikiwemo rekodi za afya, fedha, nyaraka za siri na utambulisho wa vyanzo vya habari, hazipaswi kuingizwa kwenye mifumo isiyo na ulinzi unaofaa. Nenosiri na misimbo ya usalama havipaswi kushirikishwa kabisa. Usalama hutegemea aina ya taarifa, mfumo unaotumika na namna unavyolinda faragha.

Chanzo cha siri si taarifa ya majaribio

Fikiria mtu amekutumia nyaraka kupitia WhatsApp na kukuomba usimtaje. Anaweza



kuwa mfanyakazi anayefichua ubadhirifu au shahidi wa tukio nyeti.

Kupakia ujumbe wake, jina, namba ya simu na nyaraka kwenye AI ili ikusaidie kuzielewa kunaweza kuhatarisha usalama wake.

Ondoa taarifa zinazoweza kumtambulisha, zikiwemo majina, anuani, namba za simu na utambulisho. Kumbuka kwamba hata maelezo mengine yakichanganywa yanaweza kufichua mtu.

Kanuni ni rahisi: AI isipewe taarifa nyingi kuliko inavyohitaji.

Si kila waraka unapaswa kupakiwa

AI inaweza kufupisha mikataba na ripoti, lakini si kila waraka ni salama kuupakia.

Ripoti iliyochapishwa hadharani ni tofauti na waraka uliopatikana kwa siri. Vivyo hivyo, taarifa za wagonjwa, watoto, wafanyakazi au watu wanaochunguzwa zinahitaji ulinzi maalumu.

Fahamu masharti ya faragha ya mfumo unaotumia, namna taarifa zinavyohifadhiwa na nani anayeweza kuzifikia. Ukiwa na shaka kuhusu usalama wa taarifa nyeti, usizipakie.

Toa taarifa zinazohitajika pekee

Mara nyingi AI haihitaji waraka mzima.

Ukitaka kupanga hoja, toa sehemu zisizo na utambulisho. Ukitaka kuboresha sentensi, usipakie mahojiano yote. Ukitaka maswali ya mahojiano, eleza tatizo bila kutaja chanzo.

Lengo ni kupunguza taarifa zinazoshirikishwa bila kuathiri kazi inayotakiwa.

Faragha ni haki ya kila anayehusika

Tahadhari haiishii kwa vyanzo vya siri.

Mwandishi anaweza kuwa na taarifa za umri, anuani, familia au maisha binafsi ya watu wanaotajwa kwenye habari. Kuwa na taarifa hizo hakumpi ruhusa ya kuzisambaza kwenye mifumo mingine.

Hata taarifa zitakazochapishwa baadaye zinahitaji uangalifu wakati wa kuripoti. Teknolojia mpya haiondoi wajibu wa kulinda faragha na usalama wa watu.

Na hakimiliki je?

AI imeibua maswali kuhusu matumizi ya kazi za wengine.

Mwandishi anaweza kuiomba ibadilishe maneno ya makala iliyoandikwa na mtu mwingine au itengeneze picha bila kujua chanzo chake.

Lakini kubadilisha maneno hakufanyi kazi iliyonakiliwa kuwa yako. Heshimu hakimiliki, tambua vyanzo na tumia kazi za wengine kwa mujibu wa sheria na maadili ya taaluma.

Usiipe AI nenosiri lako

Usiingize nenosiri, namba za siri, taarifa za akaunti, malipo au funguo za usalama kwenye AI.

Pia, usiitumie kama ghala la kuhifadhi nyaraka ambazo kuvuja kwake kunaweza kukuathiri wewe, chanzo chako au taasisi yako. Urahisi wa teknolojia hauondoi hatari za kufichua taarifa nyeti.

Kasi isiushinde uangalifu

AI inaweza kuokoa muda, lakini faida hiyo hupotea ikiwa chanzo kinahatarishwa, nyaraka za siri zinafichuka au faragha inavunjwa. Kabla ya kubonyeza “tuma”, jiulize: Je, mfumo huu unahitaji kweli taarifa zote hizi?

Badala ya kupakia mahojiano yenye utambulisho, unaweza kuandika: “Haya ni maelezo yaliyofichwa utambulisho. Nisaidie kupanga hoja kuu na kubaini maswali ya kufuatilia. Usibashiri majina, taasisi au maeneo.”

Hata hivyo, kuficha majina pekee hakuhakikishi usalama. Maelezo yanayobaki yanaweza kumtambulisha mtu, hivyo tathmini hatari kabla ya kushirikisha taarifa.

VISION 2050

جُمادى الأول

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama



Mbinu rahisi za kukusaidia kupata usingizi haraka



Umewahi kujikuta kitanda-ni saa sita usiku, ukigeuka upande mmoja hadi mwing-ine bila kupata usingizi? Unajifunika shuka, unaifunua, unafumba macho lakini usingizi hauji. Kadiri muda unavyopita, ndivyo unavyozidi kuwa na wasiwasi kuhusu kuamka asubuhi ukiwa umechoka.

Usingizi wa kutosha ni muhimu kwa afya ya mwili na akili. Watu wazima wengi wanahitaji angalau saa saba za usingizi kila usiku. Kukosa usingizi wa kutosha kunaweza kuathiri kumbukumbu, umakini, hisia na utendaji wa shughuli za kila siku.

Kwa mujibu wa tovuti ya afya ya Healthline, mabadiliko madogo katika tabia za kila siku yanaweza kumsaidia mtu kupata usingizi kwa urahisi zaidi. Kama una shida hiyo, jaribu mbinu hizi 8 rahisi.

Mosi, weka ratiba maalumu ya kulala na kuamka

Mwili wa binadamu una mfumo wa ndani unaoratibu muda wa kulala na kuamka. Mfumo huu hufanya kazi vizuri zaidi mtu anapofuata ratiba inayofanana kila siku.

Jitahidi kulala na kuamka muda uleule, hata siku za mapumziko. Kwa mfano, kama umezoea kuamka saa kumi na mbili asubuhi, epuka kubadilisha muda huo mara kwa mara. Pia, tenga dakika 30 hadi 45 kabla ya kulala kwa ajili ya kupumzisha mwili na akili.

Pili, acha kutumia simu kabla ya kulala

Watu wengi huingia kitandani wakiwa na simu, wakisoma ujumbe, kuangalia video au kupitia mitandao ya kijamii. Tabia hii inaweza kuchelewesha usingizi kwa sababu mwanga wa skrini huathiri uzalishaji wa homoni ya melatonin inayosaidia kudhibiti usingizi.

Aidha, taarifa na mijadala ya mitandaoni inaweza kuendelea kuuchangamsha ubongo, hivyo weka simu pembeni angalau saa moja kabla ya kulala.

Tatu, epuka kahawa na chai nyakati za jioni

Kahawa na baadhi ya aina za chai zina kafeini, kemikali inayochangamsha mfumo wa fahamu na kupunguza hisia za usingizi. Kafeini inaweza kubaki mwilini kwa saa kadhaa baada ya kunywa.

Kwa unapata shida kulala, epuka kahawa na chai yenye kafeini kuanzia alasiri, badala yake, anaweza kunywa maji au kinywaji kisicho na kafeini.

Nne, epuka kula chakula kingi muda mfupi kabla ya kulala

Kula chakula kizito na kwenda kitandani mara moja kunaweza kuleta usumbufu tumboni, kiungulia au kufanya usingizi usiwe mzuri. Jaribu kula chakula cha jioni angalau saa mbili kabla ya kulala. Ikiwa unachelewa kurudi nyumbani kutoka kazini, chagua chakula chepesi.

Tano, fanya mazoezi wakati wa mchana

Kutembea kwa kasi, kukimbia taratibu, kuendesha baiskeli au kufanya kazi za mwili kunaweza kusaidia kuboresha usingizi.

Kutembea kwa walau dakika 30 kila siku ni mwanzo mzuri. Hata hivyo, epuka mazoezi makali karibu sana na muda wa kulala ikiwa yanakufanya ushindwe kutulia.

Sita, tengeneza mazingira mazuri ya kulala

Chumba chenye joto kali, mwanga mwingi au kelele kinaweza kufanya mtu achelewe kupata usingizi.

Punguza mwanga, fungua dirisha ikiwa ni salama na mazingira yanaruhusu, na tumia matandiko yanayokufanya ujisikie vizuri. Hakikisha pia chumba kina hewa ya kutosha. Huhitaji kitanda cha gharama kubwa; usafi, utulivu na faraja vina umuhimu mkubwa.

MAKALA
SAIKOLOJIA

Na Ukhti Fatima SS
0789 201 383

Kinachovutia watu kwenye madhehebu angamizi?

Mwaka 2023, dunia ilishtushwa na vifo vya mamia ya watu katika msitu wa Shakahola nchini Kenya. Wafuasi wa mhubiri Paul Mackenzie walishawishiwa kufunga kula hadi kufa ili wakutane na Yesu mbinguni. Zaidi ya miili 430 ilipatikana, huku uchunguzi ukionyesha baadhi ya wahanga, wakiwamo watoto, walifariki kutokana na ukatili.

Miaka 23 kabla ya Shakahola, Uganda ilikumbwa na janga kama hilo. Machi 17, 2000, mamia ya wafuasi wa kundi la Movement for the Restoration of the Ten Commandments of God waliteketea ndani ya jengo la ibada huko Kanungu. Makaburi mengine ya pamoja yaligunduliwa baadaye, na idadi ya vifo ikakadiriwa kuzidi 700.

Mwaka 1978, zaidi ya watu 900 walifariki Jonestown, Guyana, kufuatia amri za kiongozi wa Peoples Temple, Jim Jones. Mwaka 1997, wafuasi 39 wa Heaven's Gate walijiua Marekani wakiamini roho zao zingesafirishwa na chombo cha angani. Majanga haya yanaibua swali: Kwa nini watu wenye akili timamu hukubali kumfuata kiongozi hadi kujitoa uhai?

Saikolojia ya kujiunga na madhehebu angamizi

Katika saikolojia na sosholojia, neno cult hutumiwa ni baadhi ya makundi yanayomzunguka kiongozi mwenye mamlaka makubwa na kudhibiti fikra, maamuzi na maisha ya wafuasi. Si kila kundi lenye imani tofauti na za wengi ni cult lakini tatizo panapotumika udanganyifu, vitisho na utegemezi kuwanyima wanachama uhuru wa kufikiri na kuamua.

Watu hawajiungi na makundi haya kwa sababu moja. Mara nyingi, mahitaji ya kawaida ya kibinadamu hukutana na mbinu za ushawishi na udhibiti. Mchakato huanza kwa ahadi zinazovutia, lakini hatua kwa hatua hugeuka utegemezi unaoweza kuwa hatari.

Mosi, hitaji la kupendwa na kukubalika. Binadamu hutamani kuwa sehemu ya jamii. Watu wanaopitia upweke, kutengwa au kuvunjika kwa mahusiano wanaweza kuvutiwa na makundi yanayowapa urafiki na upendo wa kipekee.

Waajiri wa wafuasi hutumia mbinu ya love bombing, inayohusisha kumiminia mtu sifa, upendo na uangalizi ili ajisikie amepata familia mpya. Baadaye, upendo huo unaweza kutumiwa kumdhibiti.

Pili, kutafuta maana na kusudi la maisha. Watu wanaokabiliwa na misukosuko, kufiwa au kukata tamaa hutafuta majibu kuhusu maisha na mustakabali wao. Viongozi wa cults huwavutia kwa kuahidi wokovu, mafanikio au maarifa ya siri ambayo wengine hawayajui.

Tatu, udhaifu wa kihisia na matatizo ya kiuchumi. Historia ya unyanyasaji, migogoro ya kifamilia, umasikini na mabadiliko makubwa ya maisha vinaweza kuongeza uwezekano wa kushawishiwa. Hata hivyo, elimu au akili kubwa si kinga ya moja kwa moja dhidi ya udanganyifu.

Nne, ushawishi wa mamlaka. Kiongozi anapojitangaza kuwa na uwezo wa kipekee au ujumbe maalumu kutoka kwa Mungu, baadhi ya wafuasi huamini kwamba kumhoji ni sawa na kumpinga Mungu. Hatua kwa hatua, utii huchukua nafasi ya fikra huru.

Tano, kutaka kujiona muhimu na mwenye uwezo. Makundi haya huahidi kuwafanya wanachama kuwa watu maalumu, waliochaguliwa au wenye maarifa yasiyopatikana kwa wengine. Ahadi hizo huwavutia wanaohisi hawathaminiwi katika jamii.

Sita, utegemezi na hofu ya kuondokewa. Wanachama wanapotenganishwa na familia, marafiki na shughuli za kiuchumi, hutegemea kundi kwa mahitaji yao. Vitisho, adhabu na hofu ya kupoteza wokovu huwafanya waendelee kutii hata wanapotambua udanganyifu.

Kwa nini Uislamu hauna matukio mengi ya kuogofya ya cults?

Tofauti kadhaa zinaweza kueleza namna makundi hayo yanavyojitokeza katika madhehebu tofauti.

Mosi, uhuru wa tafsiri. Baadhi ya madhehebu ya Kiprotestanti huruhusu tafsiri binafsi za Biblia na uanzishaji wa makanisa huru. Uislamu hutegemea zaidi Qur'an, Sunna na mapokeo ya wanazuoni katika kupima uhalali wa mafundisho.

Pili, wingi wa madhehebu. Mazingira yenye makanisa mengi yanayojitegemea yanaweza kurahisisha kujificha kwa makundi potofu kama taasisi nyingine za kidini.

Tatu, mipaka ya kimafundisho. Nguzo za Uislamu, misingi ya itikadi na imani kwamba Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) ni Mtume wa mwisho huweka vikwazo dhidi ya madai ya utume au mafundisho mapya.

Nne, nafasi ya viongozi. Katika baadhi ya makanisa huru, mamlaka hukusanyika kwa mhubiri mmoja mwenye ushawishi. Katika Uislamu, mamlaka ya kielimu kwa kawaida hupimwa dhidi ya maandiko na mapokeo ya wanazuoni, ingawa matumizi mabaya ya mamlaka yapo pia.

Tano, mazingira ya kisheria na kijamii. Uhuru wa kuanzisha makundi ya kidini katika baadhi ya nchi unaweza kuongeza idadi ya makundi yanayoonekana hadharani. Katika jamii nyingine, udhibiti wa kisheria na shinikizo la kijamii vinaweza kuzuia au kuficha makundi hayo.